**Watoto** 15 wazaliwa mkesha Pasaka Dar

UKURASA 5



**Mpango** naye aonya TRA kukusanya kodi kwa nguvu

UKURASA 5

Nipashe Spotika
NYOTA 10 WENYE THAMANI KUBWA ZAIDI AMERIKA KUSINI UK. 12-13





GRIEZMANN

**WACHEZAJI WA5 WANAOWEZA KUUZWA BARCA MAJIRA YA JOTO**

huyo wa zamani wa Real Betis.

**#4. SAMUEL UMTITI**

Amekuwa sehemu ya kikosi cha Barcelona tangu mwaka 2016, na kiwango cha Samuel Umtiti kimeporomoka kwa kipindi cha miezi michache iliyopita. Mshindi huyo wa Kombe la Dunia, majeruhi yamekuwa yakimwandama mara kwa mara na kusababisha kipaji chake kushuka.

Mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 27, ameanza katika mechi tano tu za ligi msimu huu.

Kuchomoza kwa walinzi vijana kama Ronald Araujo na Oscar Mingueza kumemfanya Umtiti kukosa nafasi.

Mkataba wake na Barcelona upo hadi mwaka 2023 na kwa vyovyote kuna uwezekano mkubwa akauzwa wakati wa kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

**#3. MARTIN BRAITHWAITE**

Barcelona iliishangaza dunia wakati walipomsajili, Martin Braithwaite kutoka Leganes, Februari mwaka 2020. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 raia wa Denmark, hajawa na ushawishi mkubwa kwenye kikosi hicho.

Uwapo wa Pedri na Francisco Trincao ni kigezo kingine kwa Barcelona kumuuza Braithwaite wakati wa dirisha la usajili.

**#2. PHILIPPE COUTINHO**

Uhamisho wa Philippe Coutinho kwenda Barcelona haukufanikiwa kama ilivyopangwa. Kwani ukweli ni kwamba, ameshindwa kuwa kwenye kiwango chake bora tangu aliponunuliwa kutoka Liverpool mwaka 2018.

Wakati Barcelona wakijipanga kukijenga upya kikosi hicho chini ya Rais, Joan Laporta na kocha, Ronald Koeman kuna uwezekao mkubwa wa Coutinho mwenye umri wa miaka 28, kuuzwa.

**#1. ANTOINE GRIEZMANN**

Antoine Griezmann ameshindwa kukata kiu ya mashabiki wa Barcelona pale Camp Nou.

Nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, hadi msimu huu amefunga mabao nane na kutoa pasi za mwisho sita kwenye Ligi Kuu.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, thamani yake sokoni na pale Barcelona imeshuka kwa kasi sana. Pia Griezmann na Lionel Messi hawajawa na ushirikiano mzuri dimbani jambo linalomfanya kushindwa kutamba na kung'ara.

Kwa vyovyote Barcelona itataka mshambuliaji mpya msimu ujao na inaonekana wazi kuwa Griezmann anaweza kuuzwa kipindi cha majira ya joto kinachokuja. Griezmann pia atatumika kama sehemu ya kutafuta fedha kwa Barcelona ili waweze kuingia sokoni.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa, ameshindwa kabisa kuwa kwenye kiwango chake bora alichokuwa nacho kipindi anacheza kule Atletico Madrid.

**ISIKUPITE**

SABABU kubwa ya Cristiano Ronaldo, kutokuwa na 'tattoo' yoyote mwilini mwake huku pia akiwa havuti sigara wala kunywa pombe ni kwamba anapenda kuchangia damu mara kwa mara, hivyo akijiingiza katika tabia kama hizo, hatastahili kufanya hivyo.



UKURASA 11

# Nipashe

Jumatatu Aprili 5, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580541

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

MAHUBIRI YA PASAKA

# Maaskofu wafunguka

• **Wawapasha** viongozi waliokuwa na kiburi, wahimiza amani, utulivu, wasifu ukomavu wa Watanzania... *Endelea ukurasa 2, 3, 5*

## YALIYOMO

UKURASA WA 9
**WENGI WATIBIWA KWA MISAMAHA VIJIJINI**
MUUGUZI Msaidizi wa Zahanati ya Nyakagoyahoye, Kata ya Kiluluma, Wilaya ya...

UKURASA WA 16
**ATAKA KIBANO WANAOHUBIRI UPOTOSHAJI**
SERIKALI imeombwa kuwadhibiti baadhi ya wahubiri wanaofanya mahubiri...

## Samia ahimiza kuchapa kazi

UKURASA 4



Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Thadaeus Ruwa'ichi (katikati), akiongozwa na wasaidizi wake baada ya kuendesha ibada ya Pasaka, iliyofanyika kitaifa katika Kanisa la Msimbazi Centre jijini Dar es Salaam, jana. **Picha zaidi za Pasaka uk. 18.**
**PICHA: JUMANNE JUMA**

Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play | App Store

## Wiki ngumu kwa vigogo yaja

UK.4

**MICHEZO** **AS VITA SALUTI KWA SIMBA SC** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Watanzania wahimizwa kutunza amani, utulivu

**Na Waandishi Wetu**

VIONGOZI wa dini visiwani Zanzibar, mkoani Ruvuma na Mbeya, wamewataka Watanzania kudumisha amani na utulivu kwa kuishi maisha ya kumpedeza Mungu na kujikinga na majanga mbalimbali.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa ibada ya Pasaka, Askofu wa Makanisa ya Ukombozi Pentecost Tanzania, Greenwell Kolima, alisema sikukuu hiyo inatoa nafasi kwa wakristo kutubu dhambi zao na kumrudia Mungu na kufanya yanayompendeza ikiwa ni pamoja na kuwasaidia wahitaji kama vile yatima na wagonjwa.

Kila mwaka tunasheherekea Pasaka, lakini mwaka huu ni muhimu jitafakari njia zetu na zaidi kuliombea Taifa la Tanzania, Mungu aendelee kutuepusha na majanga mbalimbali ikiwemo ajali na magonjwa," alisema Askofu Kolima.

Aliwaomba Watanzania kumwombea na kumpa ushirikiano Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan ili kuijenga nchi yenye maendeleo, haki, utawala bora na demokrasia.

**ZANZIBAR**

Visiwani Zanzibar wameungana na wakristo wengine duniani kote kusherehekea Sikukuu ya Pasaka katika hali ya amani na utulivu huku taifa likiwa na maombolezi kutokana na kifo cha aliekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli.

Mchungaji wa Kanisa la TLG, Diskon Kaganga, alisema Pasaka ya mwaka huu ni ya aina yake kutokana na kuwa na majozi makubwa ya kuondokea kwa Hayati Dk. Magufuli.

Alisema ibada za mwaka huu zimeelekeza katika maombi ya kumwombea kwa mungu amlaze pahala pema Dk. Magufuli, lakini pia kuliombea taifa kuendelea kuwa na umoja na mshikamano.

Alisema pia ibada hizo walimwomba Mungu ampe hekima na maarifa na ujasiri wa kuliongoza Taifa Rais Samia Suluhu Hassan.

Naye Mchungaji wa Kanisa la Anglikana, Godwin Emannuel, Masoud, aliwataka Watanzania kuendelea kumkumbuka Hayati Magufuli kwa sababu alikua jasiri na mwenye upendo.

Askofu wa Kanisa Katoliki Dayosis ya Zanzibar, Agostino Shao, aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona kwa kufuata maelekezo ya watalamu wa afya katika kujikinga na ugonjwa huo.

Aidha, alisema taifa lipo katika huzuni kubwa ya kuondokewa na Dk Magufuli, hivyo ni vyema kumuunga mkono Rais Samia ili kufanikisha kazi zake za kulitumikia taifa.

**TUNDURU**

Kanisa Katoliki jimbo la Tunduru- Masasi, limewaasa viongozi kushirikisha jamii katika utendaji wao hali itakayowafanya kuendelea kuishi kwa amani na utulivu wakati wote.

"Ushirikishaji husababisha amani na utulivu hata ukianzia ngazi ya familia, kaya na hata taifa huleta watu kwa pamoja na kuwafanya waishi kwa upendo," alieleza Askofu wa Jimbo hilo, Mhashamu Filbert Muhasi.

***Imeandikwa na Grace Mwakalinga, (MBEYA), Rahma Suleiman, (ZANZIBAR) na Stevie Chindiye , (TUNDURU).**



Watoto wa Kanisa Katoliki Msimbazi Center jijini Dar es Salaam wakiimba wakati wa ibada ya kuazimisha Sikukuu ya Pasaka jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Askofu Shoo awapasha viongozi wenye kiburi

**Na Waandishi Wetu**

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amesema chini ya utawala wa Rais, Samia Suluhu Hassan, wale wote waliokuwa wanajiinua na kujifanya vifutu, wakae mguu sawa, tayari kwa mwendo mbele.

Amesema ana imani hiki ni kipindi cha kuonyesha unyenyekevu na upole, lakini kusimama katika njia ambayo anataka Mungu, na kwamba jambo hilo ni nguvu kubwa sana, kuliko hata nguvu ya wale wanaojiinua na kujifanya vifutu.

Askofu Dk. Shoo, alitoa neno hilo jana katika ibada ya kwanza ya ufufuko wa Pasaka, iliyofanyika Kanisa Kuu la Usharika wa Moshi Mjini wa Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT.

Alikuwa akimshukuru Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, baada ya kutoa salaam za serikali katika kanisa hilo.

"Mama (Mghwira) nakushukuru kwa kuwa mfano, na mimi nasema chini ya mama Samia Suluhu Hassan, wale vifutu wakae mguu sawa, tayari kwa mwendo mbele.

"Wala maandiko matakatifu hayasemi hivyo, ndiyo maana mimi ni imani yangu kabisa kwamba Mungua taendelea kuwapa nguvu na wewe na wanawake, na sisi wengine kushirikiana na Mheshimiwa Rais (Samia).

**RC Mghwira: Mwanamke amepewa macho ya ndani**

Akitoa salaam za serikali katika ibada hiyo, Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira aliwaeleza waumini wa KKKT, kwamba macho ya akinababa yanachelewa kuona, lakini anashukuru Mungu macho yao yameanza kuona.

"Kwamba katika uumbaji, Mungu akampa mwanaume nguvu za mwili, akampa mwanamke macho ya ndani. Sasa nguvu za mwili na macho ya ndani vikifanya kazi pamoja vizuri, unapata manufaa makubwa sana.

"Kwa hiyo hauwezi kusema sisi ni bora kuliko wenzetu, lakini ukweli mambo ya ndani ni magumu. Mambo ya nje yanaokana, si ndiyo! ukienda kwenye kufikiri mambo ya ndani, mamcho ya ndani, utambuzi wa mambo, akina mama huenda wamepewa hiyo zaidi kuliko akina baba.

Lakini sio kwa lengo la kuumizana, ni kwa lengo la kutumia hizi karama kwa pamoja. Katika hili tutaendelea kujifunza na kuelewa jinsi inavyotupasa kuishi pamoja, kwa sababu ndivyo tulivyo."

**Askofu Minde: Kuna tunaini la Corona**

Kwa upande wake, Askofu wa Jimbo Katoliki la Moshi, Mhashamu Ludrovick Minde, akihubiri katika ibada ya Pasaka katika Parokia ya Kristo Mfalme, alisema licha ya kuwapo kwa mlipuko wa gonjwa la Corona duniani kote, na kuangamiza watu wengi, lakini bado lipo tumaini lenye kuonyesha mwanga kwa watu wote.

Kutokana na tishio la ugonjwa huo, aliwataka Watanzania kuacha hofu na kuchukua tahadhari zinazoelekezwa na wataalamu wa afya pamoja na kumrudia Mungu.

Alisema nafsi tuliyopewa ni kielezo cha kuonyesha, bado tunapaswa kufanya kazi na kumrudia Mungu ili atuvusha salama.

"Hii ni siku ya pekee kwetu, Mungu ametupa nafasi ya kuwa hai tena licha ya kuwepo kwa ugonjwa wenye hofu kubwa duniani. Huu ni wakati wakutubu na kuacha njia zetu mbaya turudie yeye," alisema Mhashamu Askofu Minde.

Katika ibada hiyo, Askofu Minde alikemea baadhi ya waamini ambao asubuhi huenda kanisani na baada ya hapo hurejea nyumbani na kuchinja mbuzi na ng'ombe za matambiko, jambo ambalo alisema sio sahihi.

"Katika Jimbo la Moshi matambiko, ushirikina, mila na desturi kandamizi za kudhulumiana ardhi na mali, baada ya moja wa wanafamilia kupoteza maisha, haya hayatavumilika wala kufumbiwa macho na kanisa," alisema

**Askofu Amani akerwa uharibifu wa mazingira**

Mkoani Arusha. Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Arusha, Mhashamu Isaac Amani, alisema uharibifu wa mazingira unaosababisha athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi zimetokana na kumkosea Mungu na kwenda kinyume na mpango wake wa uumbaji kwa wanadamu.

Askofu Amani, alikuwa akihubiri juzi usiku katika mkesha wa Pasaka katika Parokia ya Tokeo la Bwana ya Burka jijini Arusha,

Alisema mazingira pamoja viumbe ambavyo ni zawadi kutoka kwake alivyowapa wanadamu kama miti na wanyama ili wavitawale kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo, kumekuwepo na uharibifu, ambao baadhi ya maeneo yamegeuka jangwa na kusababisha mabadiliko ya hali ya hewa, kokosa mvua na mabadiliko tabia nchi.

**Askofu Konki awavaa waliowafilisi w'shara**

Mkoani Manyara. Askofu Mkuu wa Kanisa la ElimU Pentekoste Tanzania, Peter Konki, amesema baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuwakemea maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ambao wanatajwa kuua mitaji ya wafanyabiashara kwa kuwaminya kwenye kodi na kutofanya majadiliano nao, anaamini kwa sasa watabadilika.

Akihubiri katika ibada ya Pasaka katika kanisa hilo mjini Babati, Askofu Konki alisema:

"TRA walikuwa hawakai kwenye meza ya mduara na wafanyabiashara ili wajadiliane, ila kwa sasa naamini hakuna namna watafanya hivyo, kwa sababu Rais ameishaelekeza. Ili wafanyabiashara wakubali kulipa kodi bila kinyongo, ni lazima maofisa wa TRA wajenge nao urafiki, ndipo watalipa bila kusukumkwa."

**Askofu Mahimbo ataka Watanzania kujitathmini**

Mkoani Tanga. Askofu Mkuu wa Kanisa Anglikana Tanzania, William Mahimbo, akizungumza na waumini wa kanisa hilo, wakati wa ibada ya Pasaka katika Kanisa la Mt.Yohana Kristostom Nguvumali jijini Tanga, aliwataka Watanzania kujikagua ili kuona kama kweli ni weupe kama alivyokuwa Kristo katika wa mwili na roho.

Askofu Mahimbo, ambaye pia ni Askofu wa Dayosisi ya Tanga, alisema kuwa mwanadamu anapaswa kujitathmini na kukagua usafi wake kuanzia ndani ya moyo wake kabla ya kukagua usafi wa nje.

Alisema usafi ni msingi imara wa kanisa na ni vema kila mkristo akajikagua iwapo anamuishi Kristo katika maisha take ya mwili na roho.

"Tunapozungumzia weupe au usafi ni lazima tuanze kujikagua wenyewe katika maisha yetu, matendo yeti, nyumba zetu na mazingira yote tunayoishi. Tujikagua hadi kivungini mwetu ili tuone kweli tupo weupe.

***Imeandikwa na Godfrey Mushi na Mary Mosha (Moshi), Allan Isaack na Daniel Sabuni (Arusha), Jaliwason Jasson (Manyara) na Lulu George (Tanga).**

## HABARI KITAIFA

# Viongozi wa dini wasifu ukomavu Watanzania

**Na Waandishi Wetu**

VIONGOZI wa dini wamewapongeza Watanzania kwa ukomavu wa kusherehekea kumbukumbu ya ufufuko wa Yesu Kirsto, huku wakiomboleza msiba wa Hayati Rais Dk. John Magufuli.

Wamewaomba Watanzania kumuenzi kwa maneno yake ya kumuomba na kumtanguliza Mungu kila wakati katika kila jambo wanalofanya.

Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Shinyanga, Liberatus Sangu, alitoa wito huo wakati wa mkesha wa Sikukuu ya Pasaka wakati akiendesha misa kwenye Kanisa kuu la Katoliki la mama mwenye huruma lililopo Ngokolo, mjini Shinyanga.

Alisema Hayati Rais Magufuli enzi za uhai wake kila mara aliwaasa Watanzania kumtanguliza Mungu kwa kila jambo, kwasababu yeye ndiyo muweza wa yote na kuliepusha taifa na janga la virusi vya Corona na kwamba ili kumuenzi kwa vitendo inapasawa kuziishi nasaha zake.

"Hayati Magufuli hatunaye tena hapa duniani, lakini tutamtafuta kwa matendo yake na nasaha zake, hivyo ni vyema Watanzania wote tumuenzi kwa maneno yake ya kumtanguliza Mungu kwa kila jambo, pamoja na kumuombea apumzike kwa amani," alisema Sangu.

"Pia tumuombee Rais Samia Suluhu Hassan na serikali yake yote, ili wapate kutuongoza vyema katika taifa letu, pamoja na kutuletea maendeleo na kutetea haki za wanyonge," aliongeza.

KAHAMA

Waumini wa Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Karoli Lwanga, Kahama Mjini, wamesema kasi ya uongozi wa Rais Samia, haina tofauti na kasi aliyokuwa nayo Hayati Magufuli.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti baada ya ibada maalumu ya mkesha wa Pasaka iliyoongozwa na Paroko wa Parokia ya Mtakatifu Karoli Lwanga Kahama mjini, Salvatory Gwelela, mmoja wa waumini wa kanisa hilo, John Samuel alisema awali walidhani Rais Samia atakuwa na kasi ndogo katika utekelezaji wa majukumu yake, lakini kasi yake inakwenda na ya mtangulizi wake.

Alisema wanatarajia kuona miradi yote iliyokuwa imeanzishwa inasimamiwa na kukamilika, ukiwamo wa bomba la mafuta kutoka uganda hadi Tanga ili kutoa ajira kwa vijana.

Kwa upande wake, Beatrice Amoni alisema uongozi wa Mama Samia umewapatia nguvu, ujasiri na kujiamini na kwamba wanawake wanaweza kuongoza kundi kubwa la watu na kwa hatua hiyo ameanza kuichukua kubadilisha baadhi ya wizara italeta heshima ndani ya serikali yake.

"Kwa sasa mimi najiamini sana baada ya Mama Samia kuchukua nchi, ninafanya biashara zangu bila woga tofauti na kupindi cha nyuma...Tutazidi kumuombea rais wetu ili aendelee kuyaishi yale yote aliyokuwa anafanya Magufuli kipindi cha uongozi wake," alisema.

Paroko wa Parokia hiyo, Gwelela alisema kuwa mwaka jana wakati wa janga la Corona waliomba wote kwa pamoja na Mungu akawasikia na kuwaepusha na janga hilo ambalo linaendelea kuyatesa baadhi ya mataifa duniani.

DAR ES SALAAM

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, amesema kwa mara ya kwanza Pasaka ya mwaka huu, imekuwa ya kipekee wakati taifa likiomboleza kifo cha Hayati Magufuli.

Amesema hali ya utulivu wa nchi katika kuvumiliana na vipindi tofauti hususan hivi sasa, kunaonyesha ukomavu wa Tanzania katika kudumisha amani.

Askofu Malasusa aliyasema hayo jana wakati akiongoza Ibada ya Pasaka, kwenye kanisa Azania Front, jijini Dar es Salaam.

"Tulikumbushwa juzi kwa kufa kwake sisi tumepona. Lakini leo (jana) Maria Magdalena alipoenda kaburini alikuta liwazi. Pasaka ya mwaka huu ni ya pekee kwetu Watanzania.

"Kwa mara ya kwanza tunapata uzoefu wa kuondokewa na kiongozi wa nchi, tangu alipoitwa na Bwana. Utulivu na amani ambayo inaendelea nchini ni ukomavu wa taifa," alisema Askofu Malasusa.

Alisema kuwa utulivu wa Watanzania unatokana na waasisi wa taifa waliotangulia kuijenga hali hiyo na kwamba taifa litaendelea kuwa katika maombi.

"Dunia ilitikisika sana, sasa hivi dunia inapitia wakati mgumu wa magonjwa mengi hasa, corona, dunia imeendelea kugawanyika, wengi wamepoteza jamaa, uchumi umeyumba, lakini bado tunaamini Yesu aliyefufuka, ataleta suluhisho."

Kwa mujibu wa Askofu Malasusa, kifo cha Yesu na ufufuko wake ni ujumbe kwa wanadamu na kifo chake hakiishii katika kuvaa mavazi meusi, kupendezesha madhabahu.

"Sijui umekaa na huzuni kwa muda, nikwambie Pasaka ya mwaka huu ikawe suluhisho inawezekana kijana au binti umepata shida kila mchumba anayekuja unahuzunika, akiondoka bila sababu.

"Inawezekana kazini kila unapofika huna amani, kwa Pasaka hii yupo anayekuletea amani. Inawezekana unaporejea nyumbani kwako, unasikia huzuni huna amani, Pasaka hii ikawe faraja."

●**Imeandikwa na Marco Maduhu, (SHINYANGA), Christina Mwakangale (DAR) na Shaban Njia, (KAHAMA).**



# Wiki ngumu kwa vigogo yawadia

**Na Sanula Athanas,**
DODOMA

TAYARI Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari (TPA) ameshasimamishwa kazi, huku uchunguzi ukiendelea katika Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kufuatilia fedha zote zilizotolewa katika robo ya kwanza ya mwaka 2021.

Wakati Rais mpya, Samia Suluhu Hassan, akichukua uamuzi huo baada ya kukabidhiwa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2019/20, wiki hii inakwenda kuwa ngumu kwa vigogo wengi nchini pale ripoti hiyo itakapowasilishwa bungeni na kuwa wazi kwa umma.

Machi 28, mwaka huu, Rais Samia alipokea Ripoti ya CAG, Charles Kichere, Ikulu Chamwino mkoani Doroma, ikigusa maeneo mengi ukiwamo ukusanyaji wa kodi kutoka vyanzo mbalimbali, uandaaji na utekelezaji wa bajeti ya serikali, hali ya Deni la Taifa, usimamizi wa rasilimali watu, usimamizi wa mali na madeni ya serikali, na usimamizi na uendeshaji wa taasisi za umma.

Baada ya kupokea ripoti hiyo, Rais Samia, mbali na mambo mengine ikiwamo kutoa onyo kwa aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kushindwa kuzisimamia halmashauri nane zilizopata hati chafu, alitangaza kumsimamisha kazi Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Deusdedit Kakoko.

Rais Samia pia aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufanya uchunguzi BoT kufuatilia fedha zote zilizotoka katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi, mwaka huu.

Ingawa hakuweka wazi sababu za kufanyika kwa uchunguzi huo BoT, kumekuwapo na madai kwamba baadhi ya vigogo wamechota fedha kipindi ambacho mtangulizi wake Ikulu, Hayati Dk. John Magufuli, alikuwa mgonjwa.

Taratibu na sheria iliyoanzisha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, zinamtaka CAG kuwasilisha ripoti yake ya ukaguzi ndani ya siku saba za mwanzo za Bunge la Bajeti (pasi na kuzihusisha siku za mwishoni mwa wiki na sikukuu).

Bunge la Bajeti lililoanza Jumanne Machi 30, leo linaingia katika kikao (siku) chake cha nne. Ijumaa hapakuwa na kikao kutokana na Sikukuu ya Ijumaa Kuu. Kuna uwezekano mkubwa CAG akawasilisha bungeni ripoti yake hiyo wiki hii kwa kuwa hadi wiki hii inakamilika, kutakuwa na siku moja pekee (Jumatatu wiki ijayo) inayomruhusu kutekeleza wajibu wake huo wa kikatiba.

Baada ya kuwasilishwa bungeni na mawaziri husika, Ripoti ya CAG itakabidhiwa kwa kamati mbili za Bunge zenye mamlaka ya kuifanyia uchambuzi ambazo ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

Miongoni mwa hoja zinazotarajiwa kuwa gumzo katika ripoti ya CAG ni madai ya uwapo wa ufisadi katika miradi inayosimamiwa na taasisi na mashirika ya umma na 'mchwa' wa fedha za maendeleo katika halmashauri mbalimbali hasa mikoa yenye miradi mikubwa.

Hoja nyingine ni kukua kwa kasi kwa Deni la Taifa, hofu ya kuendelea kuwapo wa watumishi na wastaafu hewa, Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kujiendesha kwa hasara ya mabilioni, hali ya miundombinu ya sekta za elimu na maji.

Vilevile, Ripoti ya CAG inatarajiwa kuangazia hali ya utumishi kwa maana ya uhaba wa watumishi kwa tafsiri yake pana.



Baadhi ya wakazi wa vijiji vya Busungu na Kwikerege, Musoma Vijijini mkoani Mara, wakikinga maji baada ya kuzinduliwa kwa mradi wa maji ya bomba kutoka ziwa Victoria, jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Samia ahimiza Watanzania kuchapa kazi

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Hussein Mwinyi, wamewatumia Watanzania salamu za Sikukuu ya Pasaka.

Katika salamu hizo, wamewataka kuendelea kudumisha amani ya nchi, upendo na mshikamano na kuchapa kazi.

Viongozi hao walitoa salamu hizo kupita ukurasa zao za mtandao wa kijamii wa Instagram.

Kupitia kurasa yake ya Twitter, Rais Samia aliwataka Watanzania katika kuadhimisha sikukuu hiyo kuendelea kudumisha upendo na mshikamano.

Pia, Rais Samia aliwataka kuendelea kuijenga nchi yao kwa kuchapa kazi kwa juhudi na maarifa.

"Nawatakia Watanzania wote Pasaka njema, tuadhimishe ufufuo wa Yesu Kristo huku tukiliombea Taifa letu la Tanzania kudumisha amani, upendo na mshikamano," alisema Rais Samia.

"Tuendeleze jitihada za kuijenga nchi yetu kwa kuchapa kazi kwa juhudi na maarifa. Yesu amefufuka, Haleluya Haleluya."

Kwa upande wake Rais Mwinyi kupitia ukurasa wake wa Instagram, aliwatakia Watanzania heri ya sikukuu na kuwataka kuendelea kudumisha amani.

"Nawatakia Wanzanzibar wote na Watanzania wote kwa ujumla heri ya Sikukuu ya Pasaka. Tuendelee kudumisha amani na kuthamini amani ya nchi yetu,"alisema Rais Mwinyi.

## Mbunge mstaafu: Samia ana dhamira ya kweli

**Na Thobias Mwanakatwe**

MBUNGE mstaafu wa Jimbo la Kigamboni, Frank Magoba, amesema Rais Samia Suluhu ana dhamira ya kweli kuiletea maendeleo nchi na kumshauri kusimamia uadilifu kwa watu wote anaowaibua na kuwapa nafasi za uongozi katika serikali yake.

Pia amewashauri viongozi wa upinzani kumuunga mkono Rais Samia katika jitihada zake za kurekebisha na kubadilisha mwenendo wa siasa nchini.

"Kwa kuwa tunaamini mheshimiwa Rais Samia ni mwana demokrasia ya kweli, basi tunapaswa kumuunga mkono katika jitihada zake za kurekebisha na kubadilisha mwenendo mzima wa siasa nchini, na pale atakapoteleza basi tumshauri kwa busara na si kwa matusi, kejeli na dharau, yaliyopita si ndwele tugange yajayo," alisema.

Magoba alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uteuzi wa viongozi mbalimbali unaoendelea kufanywa na Rais Samia ambao watamsaidia katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kimaendeleo katika kipindi cha serikali ya awamu ya sita.

"Ni wazi kwamba kitu cha kwanza ambacho Mama Samia anapaswa kukifanya ili kuleta kuaminika kwa serikali yake kwa Watanzania ili kuendeleza uadilifu wa watu wote anaowaibua na kuwapa nafasi katika serikali yake," alisema.

Magoba alisema Rais Samia kwa asilimia kubwa ameiteka mioyo ya Watanzania kutokana utendaji kazi wake ambao unazingatia misingi ya demokrasia na utawala bora.

"Kiongozi wa juu wa kisiasa ni lazima ujue kusoma hali ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni kwa wakati husika. Bila kujua mahitaji ya wakati husika itakuwa ngumu kuamua aina gani ya uongozi utumie kwa ajili ya unaowaongoza," alisema.

Alisema uzoefu wa Rais Samia umempa uwanja mpana wa kuyajua hayo na kuaminika ndani ya wiki tatu za uongozi wake.

Alisema uzoefu wa Rais Samia wa kufanya kazi katika mawanda ya asasi za kiraia, kwa maana ya sekta binafsi na mashirika ya umoja wa mataifa, unampa uzoefu tofauti ya kujua mahitaji ya uongozi duniani pamoja na uzoefu wake wa kufanya kazi serikalini ndio maana anaonekana kuaminika mapema.

Magoba alisema kuna mambo makubwa matatu yanayoweza kumfanya Rais Samia aweze kukubalika zaidi na kwa haraka sana kwa watu wa kada zote;

Mosi, ni uwezo wake wa kuchukua hatua na maamuzi magumu bila kigugumizi, ni kiongozi asiyetabirika kwa kuwa kwa muda mfupi ameshawatoa jasho wateule wake na ameonekana yeye sio mfuasi wa kundi lololote ndani ya CCM.

"Kauli pamoja na matukio haya machache ndani ya kipindi kifupi cha wiki tatu yamemfanya Rais Samia Suluhu Hassan kuwa ni mtu sahihi sana kwa CCM na kwa serikali kuendeleza maono ya taifa na maono ya CCM," alisema.

Alisema ili Rais Samia aendelee kuonyesha mafanikio zaidi, ni wajibu wa kila mwananchi na wateule wake kuendelea kumpa ushirikiano.

## HABARI KITAIFA

# Ruwa'ichi awataka Watanzania kuwajali wahitaji

**Na Elizabeth Zaya**

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mwashamu Askofu, Yuda Thadaeus Ruwa`ichi, amewataka Watanzania kuwa na utaratibu wa kuwasaidia watu wenye uhitaji na wenye shida mbalimbali.

Pia, amewataka Wakristo kuwa na imani thabiti, kumkiri Kristo waziwazi, kuona umuhimu wa neno la Mungu na kuwafundisha wengine.

Akiwasilisha ujumbe wa Pasaka wa jimbo hilo wakati wa Misa Takatifu ya Pasaka katika Parokia ya Bikira Maria wa Fatima, Msimbazi Center, Askofu Ruwa`ichi, alisema ni muhimu kwa kila mwanajamii kuwakumbuka wahitaji kokote waliko.

"Mtambue kwamba tunaloadhimisha leo ni tendo kuu la huruma ya Mungu, na kutokana na tukio hili la Pasaka, sisi tumewekwa huru, tuendelee kudumu katika uhuru wa watoto wa Mungu, tujenge imani ya kuimarishana sisi sote kwa sababu hatufanani viwango vya imani, kwa ukomavu na kwa uwajibikaji wa imani, asiwepo hata mmoja ambaye atakuwa na imani legelege," alisema.

"Muwakumbuke wenzenu walio na changamoto mbalimbali, wasio na uwezo na fursa ya kufurahia matukio haya, tujitahidi kuleta faraja na kupeleka upendo kwa kila mtu. Muwe wa kujikita katika neno la Mungu ambalo lipo kwa ajili ya kutuimarisha katika imani, ufuasi na utume, tukiendelea kumshukuru Mungu, tuwaombee wakrsito katika hali zozote za maisha yao."

## Watoto 15 wazaliwa mkesha Pasaka

**Na Christina Mwakangale**

JUMLA ya watoto 15 wamezaliwa mkoani Dar es Salaam, kwenye mkesha wa Sikukuu ya Pasaka.

Kati ya watoto hao, tisa walizaliwa Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala huku sita walizaliwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Watoto sita walizaliwa MNH-Upanga pamoja na Mloganzila na kati yao wa kiume ni wanane na wakike saba.

Ofisa Habari wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), John Stephen, alisema jana kuwa watoto watano waliozaliwa siku ya mkesha huo, katika hospitali wa kike ni watatu.

Pia, katika Hospitali ya Mloganzila, kwenye mkesha huo alizaliwa mtoto mmoja wa kike.

Ofisa Habari wa MNH-Mloganzia, Neema Mwangomo, alisema mtoto huyo wa kike alizaliwa kwa njia ya upasuaji na afya ya mama na mtoto zinaendelea vizuri.

## Mpango aitaka TRA iache vitisho kwa wafanyabiashara

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amewataka watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kuacha vitisho kwa wafanyabiashara ili wafanye shughuli zao kwa uhuru.

Akitoa salamu za Sikukuu ya Pasaka jana katika Kanisa Katoliki la Mt. Paulo wa Msalaba jijini hapa baada ya kupewa nafasi ya kutoa salamu hizo na Paroko Onesmo Wisi, alisema watumishi wa TRA wanapaswa kufanya kazi kwa kufuata sheria na si kwa vitisho kwa wafanyabiashara, kwa sababu serikali inahitaji kodi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi.

"Waacheni wafanyabiashara wafanye biashara kwa uhuru kwa sababu mimi nahitaji kodi ambazo zitatumika kuendesha maisha ya Watanzania wanyonge na kuleta maendeleo ya taifa," alisema.

Aliwataka wabadhirifu wa mali za umma, kuanzia sasa wafufuke na Yesu Kristo ili wafanye kazi kwa uadilifu.

"Leo tunaadhimisha Siku ya Ufufuko wa Yesu Kristu, nawaagiza watumishi wa umma wale wabadhirifu nao wafufuke na Kristu ili waache vitendo vya ubadhirifu."

"Kama Padri alivyosema, Hayati Rais John Magufuli kiwiliwili chake ndio kimekufa, lakini matendo yake tunayaishi, vivyo hivyo watumishi na Watanzania kwa ujumla tumuenzi kwa kuyaishi yale mazuri aliyotuachia ikiwamo kufanya kazi kwa bidii," alisema.

Dk. Mpango alisema taifa ni la wanyonge linahitaji watumishi wanaofanya kazi kiadilifu ili kuleta maendeleo ya taifa na kukua kiuchumi kama alivyofanya Hayati Magufuli, wakati wa uhai wake.

"Tumetumia siku arobaini kujiandaa kiroho vivyo tuendeleze matendo mema tuliyotenda katika kipindi cha Kwaresima ili tuishi katika uadilifu kama maandiko yanavyosema," alisema Dk. Mpango.

Aliwahimiza Watanzania kumtanguliza Mungu na kumuombea kwa kuwa kazi aliyokabidhiwa sio nyepesi.

"Kila nikifikiria watu milioni 60 wananitazama mimi na ukizingatia taifa la wanyonge linahitaji kupiga hatua mbele kimaendeleo, pia tunaomba Watanzania wa dini zote kumwombea Rais Samia Hassan na serikali nzima kwa ujumla itembee katika njia ambazo Mwenyezi Mungu anapenda kwa taifa lake Tanzania lifikie."

"Mniombee na mimi sana niwe Makamu wa Rais mwaminifu, ninaye angalia haki za wanyonge wanaodhulumiwa katika nchi yetu, msiniache pekeyangu," alisisitiza. Alisema anajua Watanzania wengi walimwombea sana wakati alipoumwa, na kwamba Mungu alitaka afanye kazi yake ambayo anaifanya hivi sasa.

Katika hatua nyingine, Dk. Mpango alitoa salamu za Rais Samia kwa Wakristo na Watanzania za sikukuu hiyo huku akisisitiza washerehekee kwa amani na kuliombea taifa.


TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

P O N G E Z I

MHE. BALOZI HUSSEIN ATHUMAN KATTANGA



Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), tunakupongeza MHE. BALOZI HUSSEIN ATHUMAN KATTANGA kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Tunakutakia mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yako kwa maendeleo ya Taifa letu.

"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba msilale kazi haijaisha, sasa kajengeni heshima Misri

**TAYARI** wawakilishi wa Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, wametinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo wakiwa kinara wa Kundi A huku wakibakiza mechi moja kukamilisha hatua ya makundi.

Simba ambao wapo kundi moja na Al Ahly ya Misri, AS Vita ya DR Congo na Al-Merrikh ya Sudan, kwa sasa imebakiza mechi moja ya ugenini dhidi ya Wamisri hao itakayopigwa Ijumaa wiki hii, lakini wakiwa tayari wameshafuzu robo fainali.

Mabingwa hao wa Tanzania, Simba ambao hadi sasa wana pointi 13 kileleni, watakutana na Al Ahly, timu zote zikiwa zimefuzu hatua ya robo fainali baada ya Wamisri hao nao kufikisha pointi nane ambazo haziwezi kufikiwa na AS Vita yenye alama nne itakayokutana na Al-Merrikh Ijumaa ambayo inaburuza mkia ikiwa na pointi zake mbili.

Hivyo, katika mchezo huo utakuwa ni wakulinda heshima zaidi kwa timu zote, lakini kwa Al Ahly wakati ikihitaji kushinda ili kulipa kisasi cha kufungwa bao 1-0 katika mechi ya awali, Simba itakuwa ikipania ushindi ili kuonyesha haikubahatisha ilipoifunga timu hiyo ya Misri.

Hata hivyo, kwa upande wetu, tunaona ipo haja ya Simba kuhakikisha inashinda mchezo huo si tu kuonyesha haikubahatisha wakati iliposhinda katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ama kujenga heshima, bali kwa kushinda ugenini kutaongeza kujiamini kwa wachezaji kuelekea hatua ngumu inayofuata ya michuano hiyo.

Tunaamini kama Simba ikishinda dhidi ya Al Ahly Ijumaa, kutawafanya wachezaji kuamini hakuna kinachowazuia kupata matokeo iwe nyumbani ama ugenini wakati huu wakielekea hatua ya robo fainali.

Hatutarajii kuona wachezaji, benchi la ufundi ama viongozi wa Simba, wakipuuzia na kutofanya maandalizi ya kutosha kuelekea mchezo huo wa Ijumaa eti kwa sababu tu wameshafuzu na kuwa vinara wa kundi lao.

Matarajio yetu ni kuona yakifanyika maandalizi makubwa na tahadhari zote zikichukuliwa na wachezaji, benchi la ufundi na viongozi kama vile ndiyo kwanza inatafuta pointi muhimu zitakazofanikisha kufuzu hatua ya robo fainali.


Lakini pia tunatambua ushindi kwa Simba kutaifanya kuweka rekodi ya kwanza kwa klabu hiyo kwa kutopoteza mchezo wowote wa hatua ya makundi katika michuano hiyo msimu huu, jambo ambalo litaifanya kuzidi kuvutia wachezaji wengi wakubwa kujiunga nayo na hata wadhamini kujitokeza kuwekeza.

Itakuwa ni aibu kubwa kwa Simba ambayo hadi sasa imeruhusu mabao mawili tangu kuanza kwa michuano hiyo msimu huu, moja katika kuwania kutinga hatua ya makundi na lingine kwenye hatua ya makundi, kama itakubali kufungwa idadi kubwa ya mabao kama ilivyokuwa msimu wa 2018/19 ilipokutana na Al Ahly nchini Misri na kuchapwa 5-0.

Endapo hilo litatokea, ni wazi wachezaji watapoteza kujiamini kuelekea hatua ya robo fainali hususan wanapocheza ugenini, hivyo tunachotaka kukiona kwa Simba ni kujipanga vema ili kwenda kushinda na matokeo mabaya kwao yawe sare pekee.

Ni wakati sasa kwa Simba kuonyesha soka la Tanzania limekua kwa kutoa kichapo kwa Al Ahly nyumbani na ugenini kwani kwa kufanya hivyo, pia kutajenga heshima kwa nchi na soka la nchini hii.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kifungo Mwakalebela sawa, ila adhabu kubwa, imulikwe

Na Adam Fungamwango

**KAMATI** ya Maadili ya Shirikisho la Mpira wa Miguu wa Tanzania (TFF), imemfungia miaka mitano Makamu Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, Fredrick Mwakalebela kujihusisha na soka ndani na nje ya nchi kwa makosa ya kimaadili.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolea na TFF yenyewe ni kwamba Mwakalebela amekutana na rungu hilo zito kwa mashtaka mawili.

La kwanza ni kwamba aliitisha Mkutano wa Waandishi wa Habari Februari 19, mwaka huu na kudai kuwa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) na Kamati ya Uendeshaji wa Usimamizi wa Ligi zinahujumu timu ya Yanga, madai ambayo alishindwa kuthibitisha mbele ya kamati.

Shtaka la pili ni kwamba Mwakalebela alilalamikiwa kutoa taarifa za uongo ambapo Oktoba Mosi, 2020 aliitisha mkutano na kudai anao mkataba kati ya mchezaji Bernard Morrison na klabu ya Simba na kuuonyesha kwa waandishi wa habari huku akijua ni uongo na kitendo hicho ni kinyume cha sheria.

Katika mashtaka yote mawili, Mwakalebela ametakiwa kulipa kiasi cha Sh. milioni saba, kwani kosa la kwanza faini yake ni Sh. milioni tano na la pili ni Sh. milioni mbili.

Kwa hili niiunge mkono TFF kwani adhabu kama hii itawawafanya baadhi ya viongozi kuacha tabia ya kuongea vitu vya kufikirika, ambavyo havipo na wanachotaka ni kupunguza munkari tu ya mashabiki wao au kuwaongezea chuki dhidi ya TFF.

Kusema kweli alichofanya Mwakalebela ukitazama kwa makini utaona kuwa ni kutaka kuwatupia zigo la lawama TFF. Yaani Yanga kama haifanyi vizuri au kama haitochukua ubingwa, basi lawama badala ya kupelekwa kwa viongozi na benchi la ufundi, zielekezwe TFF. Huku ni kuichonganisha TFF na mashabiki wa Yanga. Ina maana ulikuwa ni mpango tu wa kiongozi huyo au na wenzake kukwepa lawama, lakini litatokea la kutokea.

Kuhusu la Morrison pia bado lina utata. Sitarajii eti mchezaji ambaye anacheza mpaka Ligi ya Mabingwa Afrika, achilia mbali Ligi Kuu, awe hajakamilisha usajili kwenye klabu hiyo, au eti kwenye mkataba wake hakuna saini ya klabu ambayo inaitumikia. Na bado tunaambiwa kuwa sakata lake lipo Mahakama ya Usuluhishi ya Kimataifa ya Mambo ya Michezo (CAS) hadi leo hii. Hata kwa hili bado viongozi wa Yanga wanatia shaka. Lakini pamoja na hayo yote, kwangu mimi naona kama adhabu hiyo ni kubwa mno, kuliko uhalisia wenyewe.

Ni kweli kitendo cha Mwakalebela ambaye amekuwa mara nyingi akiongea kauli tata dhidi ya TFF na klabu ya Simba, anastahili adhabu hiyo, lakini sidhani kama kumfungia miaka yote hiyo ni afya kwa maendeleo ya soka.

Nakumbuka Mwakalebela huyu huyu ndiye aliyewahi kusema kuwa Yanga imeongea na mchezaji wa Simba, Clatous Chama ikiwa na nia ya kutaka kumsajili, lakini wakati huo mchezaji akiwa kwenye mkataba na klabu yake. Nakumbuka pia Simba ilipeleka malalamiko hayo TFF na sijajua mpaka leo kama Simba ilimsamehe au la.

Pamoja na yote hayo, nilitegemea angalau mwaka mmoja tu ungemtosha kabisa kiongozi huyo kukaa nje ya uongozi wa soka na kujitafakari upya kabla ya kurejeshwa. Mara nyingi adhabu zinapotolewa hata kumchapa mtoto, lengo siyo kumuumiza au kumkomoa, bali ni kumuonya na kumkumbusha kuwa alichofanya sicho kinachotakiwa na ajirekebishe. Ni kweli kwa kosa hili Mwakalebela hakuhitaji faini peke yake, kwani amekuwa na tabia ya kujirudia ya kuongea maneno ya shutuma ambazo mara nyingi hazina ushahidi, lakini miaka mitano ni mingi na inafaa TFF iangalie na ipitie upya.

Nadhani yeye mwenyewe na klabu ya Yanga itafanya utaratibu wa kukata rufaa, ili angalau adhabu yake ipunguzwe kwa ajili ya kumfanya hata kama akirudi awe makini na anachokwenda kukisema kwenye hadhara ya watu.

Kwenye soka la sasa kitendo cha kuonyesha kuwa kuna dalili za kupanga matokeo au rushwa ni kosa kubwa, hivyo kuihusisha TFF na kitu kama hicho ni lazima ingekuja na rungu la kutaka kukomesha tabia hiyo ambayo kama ingeachiwa, basi kuna baadhi ya watu wangeanza kuichezea.

Sina ugomvi na mashabiki kwa sababu wao wana haki na uhuru wa kuongea kile wanachojisikia, lakini kwa upande wa viongozi inapaswa wawe makini sana na kauli zao, kwa sababu wao wanaaminika zaidi na wanachama na mashabiki wao.

Mwisho kabisa narudia rai yangu ya kutaka TFF iangalie upya adhabu hiyo na nadhani akikaa mwaka mmoja tu, akirejea atajirekebisha na atakuwa makini kwa kutozungumza vitu ambavyo hana uhakika navyo.

**TANGAZO**

# MINIMUM DISCLOSURE OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

NMB
Karibu yako

| S/N | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1 | **SAVINGS ACCOUNTS** | |
| | Required minimum opening balance | Business saving A/C TZS 100,000, USD 100,EUR 100,GBP 100; Bonus A/C TZS 50,000, USD 100, EUR 100 & GBP 100; Mtoto A/C TZS 7,000 or USD/EURO/GBP 5; Chipukizi A/C TZS 7,000 or USD/EURO/GBP 5; Pamoja A/C TZS 30,000 |
| | Transaction fee | N/A |
| | Monthly service fee ( break down per customer type) | FREE |
| | Statement | TZS 2000 per month |
| | Withdrawal Charges | OTC: TZS 4,000 for amount up to TZS 5Million; TZS 4,000plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Withdrawal bulky without notice | OTC: TZS 4,000 for amount up to TZS 5Million; TZS 4,000plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Cash Deposit Charge | 5% of the amount for small denomination FOREX (1,5,10 & 20) For LCYdeposit of coins 10% of the amount. |
| | Savings Card/Passbook | N/A |
| | Passbook/Card Replacement | TZS 11,800 |
| | Closing Account | TZS 9,440 USD 11.8, EUR 11.8 & GBP 11.8 |
| 2 | **CURRENT ACCOUNT** | |
| | Required minimum opening balance | Business, Supply Chain, Trade Business, Agribusiness Overdraft, Agribusiness Loans, Agri-General, Corporate, Emerging Corporate A/C - TZS 100,000, USD 100, EUR 100 & GBP 100; Personal A/C - TZS 15,000; Mwanachuo & Chapchap A/C - TZS 10,000; Wisdom - FREE; Group A/C - TZS 30,000; Fanikiwa A/C - TZS 20,000; Exclusive A/C - TZS 1Million; Executive A/C - TZS 500,000; Kilimo & Bonus A/C - TZS 50,000; Float & Scheme Financing A/C - FREE; Notice Investment A/C - TZS 500Million;Chapchap Plus (NMB Mkononi)- ZERO |
| | Monthly service fee ( break down per customer type) | Personal A/C - TZS 1,800; Business A/C & Agribusiness - TZS 15,340; Corporate, Insitution & Trade Business A/C - TZS 19,200; Exclusive A/C - TZS 35,400; Executive A/C - TZS 23,600; Emerging Corporate - TZS 19,200; Fanikiwa - TZS 2,000; Personal A/C Agribusiness - TZS 2,048; Kilimo is - TZS 1,800; for Forex A/C charges are Equivalent to TZS;Chapchap Plus (NMB Mkononi)- FREE |
| | Transaction fee | N/A |
| | Statement | TZS 2000 per month |
| | Withdrawal Charges | OTC: TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Cash Deposit Charge | 5% of the amount for small denomination FOREX (1,5,10 & 20) For LCYdeposit of coins 10% of the amount. |
| | Bank Drafts | NA |
| | Bank Drafts cancellation charge | NA |
| | Cheque book (100 leaves) | TZS 48,380 USD 35.4, EUR 23.6 & GBP 17.7 |
| | Cash Withdrawal at Counter | TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- |
| | Special Clearance | TZS 53,100 USD 52.8, EUR 46 & GBP 39.5 |
| | Cheque withdraw over the counter | TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- |
| | Dishonoured cheque | 1.5% of the amount Min 64,000 Max TZS 118,000 |
| | Cash Payment to 3rd party | N/A |
| | Cash Deposit Charge | N/A |
| | Overdrawn account interest charge | N/A |
| | Unarranged Overdraft | N/A |
| | Bulk cash Deposit | FREE |
| | Bulk cash Withdrawal | N/A |
| | Stop Payment orders | TZS 35,400, USD 23.6, EUR 17.7 & GBP 17.7 |
| | Standing Orders ( within the same bank) | FREE |
| | Standing Orders ( to other bank) | TZS 19,710 |
| | Letter of introduction | N/A |
| | Salary handling | TZS 3,540 |
| | School fees deposits | FREE |
| | TRA collection | FREE |
| | Safe custody charges | N/A |
| | Safe custody access fees | N/A |
| 3 | **EFT** | |
| (a) | Within the same bank (On Us) | FREE |
| | To other Banks ( On Others) | 2000 |
| (b) | Outward Transfers | 2000 |
| | Inward Transfers | FREE |
| 4 | **TISS** | |
| (a) | Within the same bank (On Us) | N/A |
| | To other Banks ( On Others) | TZS 10,000 |
| (b) | Outward Transfers | TZS 10,000 |
| | Inward Transfers | FREE |

| 5 | FOREIGN EXCHANGE ACCOUNT | Savings Acc | Current Acc |
|---|---|---|---|
| | Transaction fee | N/A | N/A |
| | Statement | USD 1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month | |
| | Interim statement | USD 1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month | USD1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month |
| | Withdrawal Charges | 0.25% of the amount - forex | 0.25% of the amount - forex |
| | Cash Deposit Charge | 5% for small denomination (1,5,10 & 20) | 5% for small denomination (1,5,10 & 20) |
| | Purchase/Sale of TC transactions over the counter | N/A | N/A |
| | Purchase of Foreign Cheque | N/A | N/A |
| | Sale/ Purchase of cash passport | N/A | N/A |
| | Telex/SWIFT | USD 58 | USD 58 |
| | Transfer from foreign currency denominated account to local account | N/A | N/A |
| | Outward foreign transfers | USD 58 | USD 58 |
| | Inward foreign transfers - Customers | FREE | FREE |
| 6 | **ATM CARD AND TRANSACTIONS RELATED** | | |
| (a) | Local Cards | | |
| | Issue of ATM card | N/A | N/A |
| | Replacement ATM Card (Faulty) | N/A | N/A |
| | Replacement ATM Card (Lost) | N/A | N/A |
| (b) | International Cards | | |
| | Issue of ATM card | N/A | Tanzanite - TZS 11,800; Titanium - FREE; World Reward - FREE |
| | Replacement ATM Card (Faulty) | N/A | Tanzanite - TZS 11,800; Titanium - TZS 23,600; World Reward - TZS 35,400 |
| | Replacement ATM Card (Lost) | N/A | Tanzanite - TZS 11,800; Titanium - TZS 23,600; World Reward - TZS 35,400 |
| (c) | ATM Withdrawals: | | |
| | Within the same bank (On Us) | N/A | From TZS 1,100 - 1,500 |
| | To other banks ATM (On others) | N/A | TZS 3,540 |
| | ATM mini statement | N/A | TZS 413 |
| | Bill payments through ATM | N/A | FREE |
| (d) | POS | | |
| | Within the same bank (On Us) | N/A | TZS 1,770 |
| | To other banks ATM (On others) | N/A | FREE |
| 7 | **MOBILE (SMS) BANKING** | | |
| | Balance Inquiry | N/A | TZS 400 |
| | Payments | N/A | FREE |
| | Transfers (within NMB) | N/A | FREE |
| 8 | **INTERNET BANKING** | | |
| (a) | Domestic: | | |
| | Balance Inquiry | FREE | FREE |
| | Payments | TZS 640 | TZS 640 |
| (b) | International | | |
| | Balance Inquiry | N/A | FREE |
| | Payments | N/A | FREE |
| | Transfers | N/A | USD 45 |
| 9 | **MONEY REMITTANCES** | | |
| (a) | Western Union | | |
| | Sending | N/A | N/A |
| | Received | N/A | N/A |
| (b) | Money Gram | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (c) | Coinstar | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (d) | Travelex | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (e) | Africash | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (f) | Others (Specify) | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| 10 | **BANKING SECTOR - DEPOSITS & LENDING RATES** | | |
| A | **TYPES OF LENDING RATES** | **LENDING RATES - PA (%)** | |
| | | **TZS** | **USD** |
| (a) | Flat | | |
| (b) | Declining | 17% | 9% |
| (c) | Negotiable | | |

**B — FIXED DEPOSITS**

| PERIOD | TZS | | | USD | GBP |
|---|---|---|---|---|---|
| | 500K><9.9Mil | 10M><99.9M | 100M><199M | 2000-49,999 | 2000-49,999 |
| I Month | 2.00% | 2.25% | 2.50% | 0.45% | 0.25% |
| 2 Months | 2.50% | 2.75% | 3.00% | 0.55% | 0.30% |
| 3 Months | 3.00% | 3.25% | 3.50% | 0.70% | 0.40% |
| 6 Months | 3.50% | 4.00% | 4.50% | 0.80% | 0.50% |
| 9 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 12 Months | 5.00% | 6.00% | 7.00% | 1.00% | 0.60% |
| 13-24 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 25-36 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |

**Signed By:**

**Aloyse Maro**
**Head Retail Products & Channels**

**Filbert Mponzi**
**Chief Retail Banking**




www.nmbbank.co.tz

## Angalizo matumizi mifuko ya plastiki

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WANANCHI hasa wafanyabiashara katika Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, wametakiwa kuacha mara moja matumizi ya mifuko ya plastiki kabla ya kukamatwa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Mkuu wa idara ya mazingira katika manispaa hiyo, Tambuko Joseph, alisema kuwa katazo la mifuko ya plastiki lilitolewa Mei 17, 2019 kupitia tangazo namba 394 kutokana na uwapo wa mifuko (vibebeo) iliyotengenezwa kwa malighafi ya plastiki, ambayo haikidhi viwango, lakini bado baadhi ya wananchi wameendelea kuitumia.

"Serikali iliona izuie matumizi ya mifuko hiyo na badala yake kukawa na mifuko mbadala, lakini tangu katazo hilo litolewe kumekuwa na tatizo la uingizaji wa mifuko kutoka Uganda kupitia njia za panya ambayo pia haina viwango," alisema Joseph.

Alisema agizo la Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) lililolewa Januari mwaka huu, lilitoa muda wa mwisho wa kukoma kabisa matumizi ya mifuko isiyofaa ambao umefikia kikomo Machi 31, na kwamba kuanzia Aprili 01, 2021 wangeanza msako wa kuwakamata waliokaidi.

"Sasa hakutakuwa tena na msamaha kwa watakaokamatwa, maana mbali na kufanya ukaguzi pia tumekuwa tukitoa elimu kwa wananchi kupitia makongamano, vyombo vya habari, masoko na maduka, hivyo hatutegemei kukuta bado kuna watu hasa wafanyabiashara wanatumia mifuko hiyo," alisema.

Joseph alisema kanuni ya uhifadhi wa mazingira ya kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki ya mwaka 2019 imeainisha hatua za kuchukua kulingana na mtu aliyekamatwa yupo katika kundi gani.

"Mfano wanaozalisha na kuingiza mifuko hapa nchini adhabu yao ni faini isiyopungua Sh. milioni 20 na isiyozidi bilioni moja au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja na kundi la wasafirishaji nje ya nchi adhabu yao ni Sh. milioni tano na isiyozidi Sh. milioni 20 au kifungo cha miaka miwili au vyote viwili kwa pamoja," alisema Joseph.

Alisema kuwa kundi la kuhifadhi na kusambaza mifuko adhabu yao haizidi Sh. milioni 50 au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote viwili kwa pamoja, kundi la kuuza adhabu yao ni faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. 500,000 na kundi la wanaomiliki au kutumia mifuko hiyo adhabu yao ni faini ya kati ya Sh. 30,000 na sh. 200,000 au kifungo kisichozidi siku saba au vyote viwili kwa pamoja.

Kuhusu mifuko mbadala alisema kuwa sio yote iliyoletwa baada ya katazo inafaa kwa matumizi maana ipo mingine haina vigezo, na kwamba inayofaa lazima iwe na anwani ya mzalishaji, ionyeshe mfuko una uwezo wa kubeba uzito gani na iwe na nembo ya ubora ya Shirika la Viwango (TBS).

Alisema mifuko ya plastiki ina athari nyingi ikiwamo kuchafua mazingira na kwamba utafiti umeonyesha kuwa ina uwezo wa kukaa miaka 500 bila kuoza na kuwa ikiwa mingi kwenye ardhi ulimaji unakuwa ni mgumu maana mizizi inashindwa kupita na mazao yanakauka.

Alitoa wito kwa wakazi wa manispaa hiyo hasa wafanyabiashara kutoa ushirikiano kwa kutosha kwa serikali katika kukabiliana na matumizi ya mifuko hiyo, ili kuweka mazingira salama.

# CUF yampa Samia mambo 16

**Na Romana Mallya**

CHAMA Cha Wananchi (CUF), kimeshauri mambo 16 kwa Rais Samia Suluhu Hassan, katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwamo serikali iongeze mzunguko wa fedha, kupunguza riba na kuimarisha mazingira ya kufanya biashara.

Mwenyekiti taifa wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa inabidi kuwapo na utashi wa kisiasa kutoka uongozi wa juu kuwa sekta binafsi ni muhimili muhimu wa kukuza uchumi wa nchi. Alisema kati ya mwaka 2013 na mwaka 2015, ujazi wa fedha za msingi uliongezeka kwa wastani wa asilimia 14.7

"Kati ya mwaka 2016 na mwaka 2019, fedha za msingi ziliongezeka kwa wastani wa asilimia 2.3. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi uliongezeka kwa asilimia 14.8 mwaka 2013-2015, ongezeko hilo lilipungua na kufikia wastani wa asilimia 6.4," alisema.

Alitaja jambo la pili ni kukuza demokrasia na kueleza kuwa hawawezi kujenga nchi yenye amani na maridhiano ya kweli bila kuimarisha misingi ya demokrasia na kuheshimu haki za binadamu. Pia chama hicho kimemuomba Rais Samia atumie uzoefu wake kama Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba kukamilisha mchakato wa kupata Katiba itokanayo na maoni ya wananchi.

Jambo la nne, Prof. Lipumba alilitaja ni uwekwe utaratibu wa kuwatumia wataalamu wa afya kuzifanyia uchunguzi chanjo za corona na majibu ndiyo yaongoze kuamua kuhusu kutumia au kutotumia chanjo hizo.

Alisema kwa sababu usafiri wa ndege kimataifa una ushindani mkubwa, serikali ijiimarishe safari za ndani

Pia alimuomba Rais Samia kuangalia uwezekano wa kutafuta msaada au mkopo usiokuwa na riba ili kuweza kuwezesha kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa reli ya Standard Gauge pamoja na ule wa kufua umeme mto Rufiji.

Prof. Lipumba alisema Rais Samia yupo katika kipindi cha kupendwa na kueleweka na kumuomba akitumie vizuri ndani na nje ya nchi ili awe rais wa kwanza wa Tanzania kushinda tuzo ya Mohamed Ibrahimu.




Meneja wa NMB Kanda ya Nyanda za Juu Straton Chilongola akimkabidhi Mkuu wa wilaya ya Kyela msaada wa bati 204 zenye thamani ya Sh.Mil 6.1 kwa ajili ya kuezeka majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Kyela yaliyoteketea kwa moto. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hospitali za wilaya Kyela, Chunya zasaidiwa vifaa

**Na Mwandishi Wetu,** KYELA

HOSPITALI za wilaya za Kyela na Chunya mkoani Mbeya zimekabidhiwa msaada wa vifaa vya zaidi ya Sh. milioni 15 kwa huduma za kijamii.

Vifaa hivyo ambavyo ni mabati 204 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 6 umetolewa na Benki ya NMB kwa ajili ya kuezeka majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Kyela yaliyoteketea kwa moto na vitanda 10 kwa ajili ya Kituo cha Afya Mtande Chunya vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 7.

Akipokea msaada wa mabati kwa ajili ya kuezeka majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Kyela Mkuu wa wilaya, Claudia Kitta, alisema kuwa Benki ya NMB imekuwa mstari wa mbele kwa huduma za kijamii wilayani humo. Kitta alisema mbali na msaada huo pia imeshasaidia madawati na mabati katika shule za msingi na sekondari wilayani humo jambo ambalo limekuwa likiisaidia serikali katika huduma zake za kijamii.

Naye Afisa Tawala wa Wilaya ya Chunya, Anacleth Michombero, akizungumza wakati akipokea vitanda 10 na mashuka kwa ajili ya kituo cha Mtande ameishukuru benki hiyo kwa kuendelea kusaidia huduma za kijamii wilayani humo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, John Mwanginde, alisema kuwa Benki ya NMB imekuwa mstari wa mbele kila wanapohitajika kusaidia, jambo ambalo linapaswa kuigwa na taasisi zingine za kifedha.

Akizungumza mara baada ya kumaliza ziara za Kyela na Chunya Meneja wa NMB Kanda ya Nyanda za Juu, Straton Chilongola, alisema msaada uliotolewa wilayani Kyela na Chunya ni kurejesha sehemu ya faida inayopata benki hiyo kila mwaka.

Alisema wametoa mabati 204 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 6 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Kyela na vitanda 10 na mashuka 30 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 7 kwa ajili kituo cha Afya Mtande wilayani Chunya.

HABARI KITAIFA

# Wengi watibiwa kwa misamaha vijijini

**Na Restuta Damian,** KARAGWE

MUUGUZI Msaidizi wa Zahanati ya Nyakagoyahoye, Kata Kiluluma Wilaya ya Karagwe mkoani Kagera, Winston Byaton, amesema kuna rekodi kubwa ya misamaha ya wagonjwa wanaofika kutibiwa bila fedha.

Hali hiyo inasababisha wauuguzi kufanya ufuatiliaji wa mgonjwa aliyepewa msamaha na muda wa kwenda kutafuta fedha ya kulipia deni la matibabu.

Akizungumza na Nipashe, Brayton alisema wananchi wa kijiji hicho wanakwenda kutibiwa bila kuwa na fedha zinazotakiwa,

"Unamuona kabisa hali yake sio nzuri anaweza kuwa ni ghafla au amejeruhiwa kwa ajali akaamua kuja hapa na bila kuwa na hata ile fedha angalau ya dirishani kupewa kadi kwenda kwa daktari... huyo lazima umpatie matibabu kwanza na baadae umpe gharama ili baadaye atafute," alisema Brayton.

Alisema wagonjwa wanaofika hapo ni wanafunzi, watu wazima, majeruhi, watoto chini ya miaka mitano, wazee ambao lazima uwaweke kwenye kundi maalumu endapo atashindwa kulipia.

Aidha, alisema, wauuguzi wa zahanati hiyo hulazimika kutembelea watu na kudai malipo yaliyofanyika baada ya kukaa na taarifa za mgonjwa kwa muda mrefu.

Aneth Lutainjwa, mkazi wa Kata Kiluluma, alisema kushindwa kulipia gharama za matibabu ni kutokana na jinsi hali ya uchumi wa familia ilivyo.

Alisema, kwa kushindwa kupata gharama hizo, familia hupoteza wapendwa wao hasa watoto wadogo ambao wakiugua lazima kuhangaikia zaidi upataji wa dawa.

Pius Clavery, mkazi wa kijiji Nyakagoyagoye, alisema ugonjwa hauna taarifa na upatikanaji wa pesa ni tatizo kijiji hapo, hivyo hulazimika kujitibu nyumbani kwa dawa za kienyeji.

Alisema wakazi wengi hutegemea kilimo ambacho ni cha msimu na hufanya vibarua (malipo yatokanayo kazi kwa siku) ili kupata mahitaji ya kujikimu.




Waumini wa dini ya Kikristo katika Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Masasi mkoani Mtwara, wakiwa katika ibada ya Pasaka jana katika kanisa hilo mjini Masasi mkoani hapa. **PICHA-HAMISI NASRI**.

# WETCU kupata bil. 1.2/- mwaka ujao wa fedha

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

CHAMA Kikuu cha Ushirika cha Wakulima wa Tumbaku Kanda ya Magharibi (Wetcu 2018 Ltd), kinatarajia kupata jumla ya Sh. bilioni 1.2 kutoka vyanzo mbalimbali katika mwaka ujao wa fedha.

Taarifa hiyo ilitolewa na Meneja Mkuu wa WETCU 2018 Ltd, Samwel Jokeya, wakati akiwasilisha mapendekezo ya makisio ya mapato na matumizi ya mwaka 2021/22 wakati wa Mkutano Mkuu wa Wetcu 2018 Ltd), wa 28.

Alisema wanatarajia kupata Sh. milioni 814.6 ambazo ni ushuru wa tumbaku kilo milioni 14.4 zitakazouzwa kwenye vyama vya ushirika vya Msingi, kwenye pango la nyumba , ofisi na maghala wanatarajia kupata Sh. milioni 43.5.

Jokeya alisema mapato mengine yatatokana na gawio la faida ya hisa kutoka Benki ya CRDB ambapo watapata Sh. milioni 408 na gawio la faida kutoka FDR Exim Bank ya Sh. milioni 13.9.

Baada ya mapendekezo hayo, wajumbe wa mkutano huo walipitisha bajeti hiyo kwa ajili ya mwaka ujao wa fedha.

Katika hatua nyingine, mkutano huo umewachagua mwenyekiti na wajumbe wa bodi watakaosimamia ushirika kwa kipindi cha miaka mitatu.

Akitangaza matokeo Mrajis Msaidizi Mkoa wa Tabora, Absalom Cheliga, alisema nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi aliyechaguliwa ni Hamza Kitunga na Makamu Mwenyekiti Mariam Mayoba.

Alisema wajumbe wengine wa Bodi ya WETCU waliochaguliwa ni Mussa Maganga, Salum Kamwezi, Salum Msensemi, Erick Martin, Ally Ally na kwa upande wa uwakilishi alichaguliwa Stephen Kitevi.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati akifungua mkutano huo, uliwataka wajumbe kuhakikisha wanachagua viongozi waadilifu, waaminifu ambao watasaidia kuupeleka mbele ushirika na kuinua maisha ya wakulima.

Alisema viongozi ni lazima wawe na shamba ambao watatumia fursa yao kuwatetea wakulima kwa kuwa nao watakuwa sehemu yao

# Klabu ya pombe karibu na shule yakera kijijini

**Na Christina Haule,** KILOSA

WANAVIJIJI wa Kata ya Ulaya wilayani Kilosa mkoani Morogoro wameiomba serikali kuingilia kati suala la ujenzi wa kilabu cha pombe karibu na shule.

Lengo ili kuwaepusha wanafunzi kuiga na kuona sawa kuishi na mitazamo hasi wanayoiona kutoka kwa walevi wanapopita wawapo katika masomo kwenye Shule ya Msingi Ulaya.

Mmoja wa wanakijiji cha Ulaya Mbuyuni, Abdulahman Mgawe, alisema hayo jana wakati taasisi isiyo ya kiserikali inayojihusisha na utoaji wa elimu DIRA Organization ilipofanya kikao na wadau wa elimu wilayani humo chini ya mradi wa kusimamia na kufuatilia matumizi ya Rasilimali za Umma (PETS) unaofadhiliwa na Shirika la The Foundation For Civil Society (FCS).

Mgawe alisema awali shule ilikuwa ikimiliki eneo lote peke yake, lakini baadaye kuliibuka maslahi ya kisiasa yaliyopelekea eneo hilo kumegwa na kutakiwa kuwa soko, lakini baadaye yakabadilishwa uamuzi na kuwekwa kilabu cha pombe za kienyeji.

Alisema kilabu hicho cha pombe za kienyeji ambacho kinafanya kazi kila siku kimekuwa kikileta shida kwa wanafunzi kwa sababu walevi wamekuwa wakifanya tabia za ajabu, ikiwamo kukojoa maeneo yasiyostahili, kutokana na pengine kusogelea maeneo ya shule, jambo ambalo limekuwa ni tatizo kwa wanafunzi.

Alisema kilabu hicho kipo umbali wa kilometa 20 hadi 30 na ilipo shule hiyo ya msingi, jambo ambalo litawafanya wanafunzi wanaosoma shuleni hapo kuiga tabia za wazazi au wakubwa wanaowaona wakitoka kwenye kilabu hicho wakiwa wamelewa.

Hivyo Mgawe aliomba serikali kurejesha eneo hilo mikononi mwa shule, na kwamba kama wanalitaka eneo hilo basi wabadilishe matumizi.

Akifunga kikao hicho, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Katabaro Rwegelela, aliwataka watendaji wa kata kuhakikisha wanabeba majukumu yao na kuwasilisha changamoto zinazojitokeza mapema kwa serikali ili zitatuliwe na kusaidia watoto.

Rwegelela alisema ni jambo jema kwa watendaji wa kata sasa kushirikiana na wadau wa elimu wa ngazi za chini katika kuboresha upungufu unaojitokeza.

# Watendaji wapewa jukumu chakula shuleni

**Na Christina Haule,** KILOSA

WATENDAJI wa kata na vijiji wilayani Kilosa mkoani Morogoro, wametakiwa kusimamia uzalishaji wa mazao ya chakula na kuhakikisha watoto wa shule zote za msingi na sekondari wanapata chakula wawapo shuleni.

Imeelezwa kuwa ni aibu wilaya inayotoa chakula kwa wingi kushindwa kulisha wanafunzi.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Katabaro Rwegelela, alisema hayo wakati akifungua kikao cha wadau wa elimu wilayani humo kilichosimamia mpango wa kusimamia na kufuatilia matumizi ya rasilimali za Umma (PETS) kilichoandaliwa na taasisi isiyo ya kiserikali inayojihusisha na masuala ya kutoa elimu kwa jamii DIRA kwa ufadhili wa The Foundation For Civil Society (FCS) kilichofanyika wilayani Kilosa mkoani Morogoro.

Rwegelela alisema ni aibu kwa wilaya kama Kilosa kushindwa kulisha watoto chakula shuleni wakati ndio wilaya ambayo inatoa chakula kingi shambani ikiwamo mpunga na mahindi.

Alisema wakati umefika sasa wa viongozi wa kata na vijiji kuwaelimisha wananchi kuona umuhimu wa kuchangia suala la chakula mashuleni bila kuleta shida kwa sababu wilaya haina tatizo la ukosefu wa chakula.

Naye Mkurugenzi wa DIRA, Erasmo Tullo, alisema matokeo ya kuimarika kwa uwazi, uwajibikaji na ubora wa huduma kunaonekana kwa sasa, na kwamba hayo ni matunda yanayoongeza chachu ya ushirikishwaji wa wananchi katika suala zima la maendeleo.

Tullo alisema wanavijiji wameonekana kuanza kuelimika na kuchangia kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ya vijiji huku wakizijua haki zao katika kusimamia rasilimali za Umma.

Alisema uchangiaji wa wananchi katika shughuli za maendeleo umeonyesha mwanga wa maendeleo katika vijiji vya mradi vilivyopo kwenye kata tano za wilaya hiyo, na kwamba uchangiaji huo umeondoa changamoto mbalimbali za kielimu.

Naye Mkaguzi wa Ndani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, Eliuta Makugira, aliwataka viongozi wa kata na vijiji wilayani humo kusimamia na kuweka sawa changamoto za maeneo yao kupitia mikutano mikuu bila kutegemea uongozi ngazi ya wilaya au mkoa ili kuepusha migogoro inayojitokeza mara nyingi katika vijiji.

Hata hivyo alisisitiza watendaji na wenyeviti wa vijiji kuona namna ya kuwaeleza wananchi kuongeza kasi ya uchangiaji wa miradi ya maendeleo ya vijiji ikiwamo ujenzi wa madarasa na shule za mikondo huku wakizingatia kumalizia ujenzi hadi hatua ya mwisho.

Alisema mpaka sasa yapo maboma mengi yamebaki wazi yakisubiri serikali kupitia halmashauri kumalizia huku halmashauri hizo zikiwa bado hazina fedha za umaliziaji.

Alikemea tabia ya walimu kukataa kukaa kwenye nyumba zao zilizojengwa jirani na shule ambapo alisema kukaa mbali kwa walimu kunachangia kushuka kwa kiwango cha taaluma cha mwanafunzi.

Mmoja wa wakazi wa Kata ya Zombo, Rajabu Tegamwili, aliishauri serikali kuendelea kuwahimiza walimu kukaa kwenye nyumba zilizojengwa kwa nguvu za wananchi ambapo alisema kutokaa kwenye nyumba hizo na kuziacha zikichakaa bila matumizi ni ubadhilifu wa matumizi ya Rasilimali za Umma.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk Damas Ndumbaro (kulia), akiteta jambo na Kamishna Uhifadhi wa TFS pamoja na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa (katikati), wakati wa kikao kifupi cha kupata tathmini ya maendeleo ya ung'oaji miti katika eneo litakalochimbwa bwawa la kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere (JNHPP).

# Wananchi wajitolea kujenga zahanati

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wa Kijiji cha Nyaligongo wilayani Shinyanga, ambao wanajishughulisha na uchimbaji wa madini ya dhahabu, wamejitolea kuanza ujenzi wa zahanati ili kuondokana na adha ya kufuata huduma ya matibabu umbali mrefu.

Mwenyekiti wa kijiji hicho Masumbuko Lushona, alisema juzi kwenye ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, ambaye alifika kukagua ujenzi wa zahanati hiyo, kuwa baada ya kuona wanapata shida ya matatibu ndipo wakachangishana fedha ili kuanza ujenzi.

Alisema wananchi wa kijiji hicho hua wanafuata huduma ya matibabu umbali wa kilomita tano katika kijiji jirani cha Mwakitolyo, huku baadhi ya kinamama wakijifungulia jiani, lakini kukamilika kwa zahanati hiyo itawaondolea changamoto hizo na kuimarisha afya zao.

"Wakazi wa Kijiji hiki cha Nyaligongo shughuli zao kubwa ni uchimbaji wa madini ya dhahabu, hivyo hatushindwi kujenga zahanati, na sasa tupo katika hatua ya msingi na hadi kufika mwishoni mwa mwaka huu itakuwa imeshakamilika na makisio yetu itagharimu Sh. milioni 90," alisema Lushona.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Hoja Mahiba, aliwapongeza wananchi hao kwa kuanzisha ujenzi huo wa zahanati, na kubainisha kuwa Sera ya afya inasema kuwapo na zahanati kwa kila kijiji, na miradi hiyo huwa inaibuliwa na wananchi wenyewe, kisha serikali inawaunga mkono kuikamilisha.

Kwa upande wake Mboneko, alisema ni jambao jema wananchi hao kujitolea kuchangia shughuli za maendeleo wenyewe, kwa kutatua changamoto zao kuliko kuitegemea serikali kwa kila kitu, na kuahidi kuwaunga mkono hadi zahanati hiyo itakapoanza kutoa huduma ya matibabu.

Mmoja wa kinamama wa kijiji hicho, Mary Benjamin, walisema ujenzi wa zahanati hiyo utakuwa msaada kwao, na kueleza kuwa huduma ya matibabu inapokuwa mbali wanaoteseka ni wanawake na watoto.

# Wachimbaji wa dhahabu wajenga kituo cha polisi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WACHIMBAJI wa dhahabu katika machimbo ya Mwakitolyo wilayani Shinyanga, wamechangishana fedha na kujenga kituo cha Polisi ili kukabiliana na uhalifu kwenye ikiwamo kuporwa mali zao.

Mwenyekiti wa wachimbaji hao, Alphonce Paulo, akizungumza juzi kwenye ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko ya kukagua ujenzi huo kwenye maeneo ya machimbo ya dhahabu, alisema kuwa baada ya kukithiri kwa uhalifu na usalama wao kuwa mdogo ndipo wakaona kuna umuhimu wa kituo hicho.

Alisema waliitana kwenye mkutano na kujadili suala la ujenzi wa kituo hicho, ambapo wazo hilo awali lilitolewa na DC Mboneko, kuwa ili wawe salama na mali zao, ni lazima waanzishe ujenzi wa kituo cha Polisi, ndipo wakaanza kuchangisha fedha na sasa ujenzi upo kwenye ufungaji renta.

"Ukosefu wa kituo cha polisi kwenye maeneo haya ya machimbo ya dhahabu ni hatari sana, lakini kituo hiki kitakapokamilika kujengwa ambapo matarajio yetu hadi mwishoni mwa mwezi huu kiwe tayari, kitakuwa msaada mkubwa sana kulinda usalama wetu na mali zetu," alisema Paulo. Naye Mkuu wa Polisi Wilaya ya Shinyanga, John Kafumu, alisema kwenye machimbo hayo kuna uhalifu mkubwa yakiwamo mauaji ya kukatwa mapanga, lakini kituo hicho kitakapokamilika kitapunguza matukio hayo, sababu askari watakuwa doria saa 24 ili kuhakikisha amani inatawala. Kwa upande wake DC Mboneko, alisema kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho, kitatoa fursa pia kwa wafanyabiashara kwenda kuwekeza kwenye maeneo hayo, zikiwamo na taasisi za kifedha kuwasogezea huduma karibu sababu ya kuwapo amani.

Alisema maeneo ambayo hakuna amani hapawezi kuwa na maendeleo, lakini kituo hicho cha polisi kitafungua milango ya maendeleo, na kuwataka wachimbaji hao waendelee kuchangisha fedha hadi kukikamilisha, huku akiwapatia Sh. milioni 10, ambazo aliziomba kutoka Mamlaka ya mapato Tanzania TRA ili kuwaunga mkono.

Katibu msaidizi wa umoja wa wachenjuaji wa madini ya dhahabu Mwakitolyo, Elisha Rugwisha, akisoma taarifa ya ujenzi huo wa kituo cha polisi, alisema ulianza Februari mwaka huu na sasa upo katika hatua ya renta, na unatarajiwa kukamilika mwezi huu kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 30.

Nipashe
Spotika




NYOTA 10 WENYE THAMANI KUBWA ZAIDI AMERIKA KUSINI UK. 12-13



GRIEZMANN

# WACHEZAJI WA5 WANAOWEZA KUUZWA BARCA MAJIRA YA JOTO

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA itakuwa na msimu wa aina yake wa kipindi cha usajili wa majira ya joto. Huku majaliwa ya Lionel Messi yakiwa bado hayajulikani, janga la virusi vya corona limewaumiza kiuchumi miamba hao wa Catalunya.

Hivyo, kwenye dirisha hilo la usajili watalazimika kutumia akili zaidi na mojawapo ni kuuza wachezaji kadhaa ili kupata fedha za kuimarisha kikosi chao.

Kocha Ronald Koeman na Rais mpya, Joan Laporta, watahitaji kupata wachezaji wapya wa kuiwezesha Barcelona kutamba msimu ujao.

Makala haya yanawaangalia wachezaji watano ambao wanaweza kuuzwa kipindi cha majira ya joto, twende sasa...

**#5. JUNIOR FIRPO**

Mmoja wa wachezaji ambaye mara kwa mara amekuwa akihusishwa kuondoka Barcelona ni Junior Firpo. Mlinzi huyo wa Hispania bado hajawa na nafasi kwa kocha, Ronald Koeman.

Mlinzi huyo wa kushoto amecheza mechi sita tu na 'Blaugrana' kwenye ligi msimu huu, huku nne kati ya hizo akitokea benchi. Akiwa bado ana umri wa miaka 24, Firpo ana nafasi ya kutamba kwenye timu nyingine Ulaya.

Mambo yanaonekana kuwa magumu pale Camp Nou na kuondoka hapo Barcelona kunaweza kufufua kipaji cha beki huyo wa zamani wa Real Betis.

**#4. SAMUEL UMTITI**

Amekuwa sehemu ya kikosi cha Barcelona tangu mwaka 2016, na kiwango cha Samuel Umtiti kimeporomoka kwa kipindi cha miezi michache iliyopita. Mshindi huyo wa Kombe la Dunia, majeruhi yamekuwa yakimwandama mara kwa mara na kusababisha kipaji chake kushuka.

Mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 27, ameanza katika mechi tano tu za ligi msimu huu.

Kuchomoza kwa walinzi vijana kama Ronald Araujo na Oscar Mingueza kumemfanya Umtiti kukosa nafasi.

Mkataba wake na Barcelona upo hadi mwaka 2023 na kwa vyovyote kuna uwezekano mkubwa akauzwa wakati wa kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

**#3. MARTIN BRAITHWAITE**

Barcelona iliishangaza dunia wakati walipomsajili, Martin Braithwaite kutoka Leganes, Februari mwaka 2020. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 raia wa Denmark, hajawa na ushawishi mkubwa kwenye kikosi hicho.

Uwapo wa Pedri na Francisco Trincao ni kigezo kingine kwa Barcelona kumuuza Braithwaite wakati wa dirisha la usajili.

**#2. PHILIPPE COUTINHO**

Uhamisho wa Philippe Coutinho kwenda Barcelona haukufanikiwa kama ilivyopangwa. Kwani ukweli ni kwamba, ameshindwa kuwa kwenye kiwango chake bora tangu aliponunuliwa kutoka Liverpool mwaka 2018.

Wakati Barcelona wakijipanga kukijenga upya kikosi hicho chini ya Rais, Joan Laporta na kocha, Ronald Koeman kuna uwezekao mkubwa wa Coutinho mwenye umri wa miaka 28, kuuzwa.

**#1. ANTOINE GRIEZMANN**

Antoine Griezmann ameshindwa kukata kiu ya mashabiki wa Barcelona pale Camp Nou.

Nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, hadi msimu huu amefunga mabao nane na kutoa pasi za mwisho sita kwenye Ligi Kuu.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, thamani yake sokoni na pale Barcelona imeshuka kwa kasi sana. Pia Griezmann na Lionel Messi hawajawa na ushirikiano mzuri dimbani jambo linalomfanya kushindwa kutamba na kung'ara.

Kwa vyovyote Barcelona itataka mshambuliaji mpya msimu ujao na inaonekana wazi kuwa Griezmann anaweza kuuzwa kipindi cha majira ya joto kinachokuja. Griezmann pia atatumika kama sehemu ya kutafuta fedha kwa Barcelona ili waweze kuingia sokoni.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa, ameshindwa kabisa kuwa kwenye kiwango chake bora alichokuwa nacho kipindi anacheza kule Atletico Madrid.

## ISIKUPITE

SABABU kubwa ya Cristiano Ronaldo, kutokuwa na 'tattoo' yoyote mwilini mwake huku pia akiwa havuti sigara wala kunywa pombe ni kwamba anapenda kuchangia damu mara kwa mara, hivyo akijiingiza katika tabia kama hizo, hatastahili kufanya hivyo.



NIPASHE JUMATATU APRILI 5, 2021





# NYOTA 10 WENYE THAMANI KUBWA ZAIDI AMERIKA KUSINI

**LONDON,** England

WACHEZAJI wa kutoka bara la Amerika Kusini ni moja ya nyota bora kabisa duniani. Nchi za kutoka bara hilo kwa uhakika kabisa zinapenda sana soka.

**Brazil, Argentina na Uruguay kwa sasa ndio timu za taifa zenye vikosi bora zaidi, huku zote zikiwa kwenye 10-bora ya orodha ya viwango vya Shirikisho la Soka la Kimataifa, Fifa.**

Wachezaji kutoka huko, ndio nyota wakubwa zaidi barani Ulaya na wameshinda mataji mengi wakiwa na klabu zao. Hivyo ni kawaida wachezaji kutoka Bara la Amerika Kusini kuwa na thamani kubwa duniani.

Makala haya yanawaangalia wachezaji 10 wa Amerika Kusini ambao wana thamani kubwa zaidi kwa sasa duniani, hawa hapa...

### #10. JOSE MARIA GIMENEZ | URUGUAY | ATLETICO MADRID – EURO MIL. 65

Mmoja kati ya walinzi wawili tu kwenye orodha hii Jose Maria Gimenez wa Uruguay anayeichezea miamba ya soka la Hispania, LaLiga, Atletico Madrid.

Mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 26, alijiunga na klabu hiyo kwa ada ya euro milioni 900,000 kipindi cha majira ya joto mwaka 2013. Mlinzi huyo wa kati amekuwa akisumbuliwa na majeraha katika kipindi cha hivi karibuni, lakini amekuwa nguzo imara kwa Atletico Madrid kwa miaka mingi. Gimenez kwa sasa thamani yake ni euro milioni 65.

### #9. FEDERICO VALVERDE | URUGUAY | REAL MADRID – EURO MIL. 70

Federico Valverde ni mchezaji wa Real Madrid ya Hispania na kiungo huyo mwenye umri wa miaka 22, aling'ara zaidi msimu wa 2019-20 wakati 'Los Blancos' hao wakishinda taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga. Valverde pia amekuwa sehemu ya kikosi cha Uruguay tangu mwaka 2017 na mara zote yupo kikosi cha kwanza kwa 'La Celeste' hao.

Kwa sasa anafurahia maisha yake mbele ya goli, licha ya kuwa amecheza mechi 15 tu kwenye LaLiga, msimu huu nusu ya mechi hizo akitokea benchi. Fede Valverde ana mabao matatu kwa jina lake na thamani yake ni euro milioni 70.

### #8. MARQUINHOS | BRAZIL | PARIS SAINT-GERMAIN – EURO MIL. 70

Mlinzi wa pili kuwapo kwenye orodha hii ni beki wa Paris Saint-Germain, Marquinhos. Marquinhos amekuwa na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, tangu mwaka 2013, akijiunga nao kutoka AS Roma kwa euro milioni 31.4 akiwa na umri wa miaka 19.

Baada ya kuondoka kwa Thiago Silva kipindi cha majira ya joto kilichopita, Marquinhos sasa ni mchezaji nguzo kwa PSG.

Kwa sasa, Marquinhos ambaye ameichezea timu ya Taifa ya Brazil meci 51, thamani yake ni euro milioni 70.

### #7. CASEMIRO | BRAZIL | REAL MADRID – EURO MIL. 70

Kwa sasa Casemiro anacheza pale Real Madrid katika nafasi ya kiungo mkabaji. Ni mmoja wa viungo bora kabisa duniani.

Casemiro kwa sasa thamani yake inatajwa kuwa euro milioni 70 na sokoni yupo nyuma ya nyota wa Bayern Munich, Joshua Kimmich kama viungo bora wakabaji duniani.

### #6. LAUTARO MARTINEZ | ARGENTINA | INTER MILAN – EURO MIL. 70

Straika Lautaro Martinez anacheza pale Inter Milan ya Italia na amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia sana.

Martinez alikuwa na mwanzo mzuri pale kwenye dimba la San Siro na tayari amefunga mabao 30 kwenye Serie A kwa 'Nerazzurri' hao. Na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ni mmoja wa mastraika bora wanaotamba Ulaya.

Alijiunga na miamba hao wa Italia kipindi cha majira ya joto mwaka 2018 kwa ada ya euro milioni 22.7. Martinez anatarajiwa kusaini mkataba mpya na Inter Milan, ambao utakuwa na kipengele cha kumuuza kwa euro milioni 111. Hata hivyo, thamani yake sokoni ni euro milioni 70.

### #5. PAULO DYBALA | ARGENTINA | JUVENTUS – EURO MIL. 70

Paulo Dybala alikuwa anatajwa kama mmoja wa wachezaji atakayeiteka dunia kwa misimu kadhaa iliyopita. Lakini kwa sasa kipaji chake kimeshindwa kuthibitisha hilo.

Mshambuliaji huyo kwa sasa hajawa kwenye ubora wake baada ya kufunga mabao kadhaa kwa kipindi cha msimu wa 2019-20.

Dybala amekuwa na Juventus tangu mwaka 2015 akicheza mechi 244 katika mashindano yote na kufunga mabao 98 na pasi za mwisho 40 kwa klabu hiyo. Usajili wa mchezaji huyo umekuwa gumzo kwa misimu miwili iliyopita na kwa sasa thamani yake ni euro milioni 70.



NEYMAR

### #4. ROBERTO FIRMINO | BRAZIL | LIVERPOOL – EURO MIL. 72

Roberto Firmino ni mchezaji wa Liverpool, ambaye alishinda taji la Ligi Kuu England msimu uliopita.

Firmino amekuwa nguzo muhimu kwa kikosi cha kocha Jurgen Klopp, kwani amekuwa msaada mkubwa kwa Mohamed Salah na Sadio Mane.

Firmino alijiunga na Liverpool kipindi cha majira ya joto mwaka 2015, kwa euro milioni 33. Kwa Firmino ambaye atatimiza umri wa miaka 30 baadaye mwaka huu, thamani yake inatajwa kuwa ni euro milioni 72.

### #3. ALISSON BECKER | BRAZIL | LIVERPOOL – EURO MIL. 80

Magolikipa mara zote hawapewi thamani kubwa, lakini golikipa namba moja wa Liverpool, Alisson ni mmoja wa wachezaji wenye thamani kubwa duniani kwa sasa.

Alikuwa golikipa ghali zaidi wakati alipojiunga na Liverpool mwaka 2018 kutoka AS Roma kwa euro milioni 62.5. Alishinda tuzo ya golikipa bora wa mwaka wa Fifa mwaka 2019 na ameshinda taji la Ligi Kuu England na Ligi ya Mabingwa Ulaya na sasa thamani yake ni euro milioni 80.

### #2. LIONEL MESSI | ARGENTINA | BARCELONA – EURO MIL. 80

Lionel Messi ni mmoja wa wachezaji bora kabisa kuwahi kutokea kwenye soka duniani. Ingawa sasa umri wake unamtupa mkono, lakini bado ni mchezaji bora kabisa.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or anachukua nyumbani euro milioni 138 kila mwaka akiwa na mshahara wa uero 500,000 kwa wiki.

Kwa sasa akiwa na umri wa miaka 33, thamani yake inatajwa kuwa euro milioni 80.

### #1. NEYMAR | BRAZIL | PARIS SAINT-GERMAIN – EURO MIL. 128

Mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi Amerika Kusini kwa sasa ni nyota wa Paris Saint-Germain, Neymar. Alisajiliwa kwa euro milioni 222 kutoka Barcelona kwenda PSG mwaka 2017.

Neymar amekuwa na wakati mzuri kwa miamba hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, akifunga mabao 83 na kutoa pasi za mwisho 46 katika mechi 102 kwenye mashindano yote.

Majeruhi ya mara kwa mara yamekuwa yakimsumbua na hivyo kujikuta akilazimika muda mwingi kuwa nje ya dimba.

Aliisaidia PSG kutwaa taji lao la Ligi Kuu msimu uliopita na kuwawezesha kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza.

## Nukuu

"Tunafuraha sana si tu kwa sababu tumefuzu, lakini pia tumecheza mechi nzuri sana. Tungeweza kufunga zaidi kwa sababu tulitawala mchezo, lakini tumeridhishwa kwa kufuzu hatua ya robo fainali [ya Ligi ya Mabingwa Afrika] na tumemaliza katika nafasi ya kwanza," **Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes baada ya kuifumua AS Vita ya DR Congo mabao 4-1 juzi.**




"Klabu za Tanzania kwa sasa zina pesa kuliko klabu za DR Congo, ndio maana wachezaji wazuri wanakimbilia Tanzania," **Kocha Mkuu wa AS Vita, Florent Ibenge, baada ya timu yake kukubali kipigo cha mabao 4-1 kutoka kwa Simba kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika juzi**



"Wacha tu niseme, nimehamasika kipekee kushinda mchezo huu na kutinga nusu fainali. Kinachoendea sasa hakitabadilisha matokeo ya fainali pale Kiev. Hiyo ni zamani, kwa hivyo sifikirii kuhusu hilo. Ninafikiria kuhusu timu. Kila mtu anazingatia timu yake na kila mtu anataka kushinda hiyo mechi. Tangu wakati huo, tumeshinda Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa. Sisi ni washindi. Hayo ni mabadiliko makubwa," **Mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, baada ya kuulizwa kuhusu kukabiliana tena na Real Madrid na beki Sergio Ramos kwenye Ligi ya Mabingwa.**



Nipashe Spotika




# SIMBA YATINGA ROBO CAF NA REKODI KIBAO

**Na Adam Fungamwango**

DAKIKA 90 za mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya Simba na AS Vita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, zilihitimishwa kwa wenyeji kushinda mabao 4-1.

**Ilikuwa ni furaha kwa mashabiki na wanachama wa Simba ambao walikula Sikukuu ya Pasaka kwa raha kutokana na si ushindi tu, bali mpira safi ambao wameubatiza jina la 'soka biriani'.**

Ni ushindi ambao umeipeleka Simba kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku ikiweka rekodi kibao na wachezaji wa timu hiyo pia wakiweka rekodi za aina yake, hapa tunazianika...

### #1. KUIFUNGA TENA AS VITA NA KUTINGA ROBO FAINALI

Simba imerudia kile ilichokifanya Machi 16, 2019, ilipotinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa kwa kuifunga timu hiyo hiyo ya AS Vita mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa. Mwaka huu pia AS Vita imekuwa ngazi ya Simba kwenda robo fainali kwa mara nyingine tena kwa kuchapwa idadi hiyo ya mabao.

### #2. KUONGOZA KUNDI A

Kwa mara ya kwanza, Simba imekuwa kinara kwenye makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika. Kwa ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya AS Vita, imeongoza Kundi A ikiwa na pointi 13, ikicheza mechi tano, kushinda nne na sare moja, ikifunga mabao tisa na kufungwa moja.

Hata kama itafungwa kwenye mechi ya mwisho dhidi ya Al Ahly, Aprili 9, mwaka huu ugenini, bado Simba itaendelea kuongoza kundi hilo, kutokana na ukweli kwamba Wamisri hao ambao nao tayari wametinga hatua ya robo fainali, wana pointi nane, hivyo hata wakishinda wataishia na pointi 11.

### #3. MIQUISSONE HATARI KWA MKAPA

Bao lililofungwa na kiungo mshambuiaji wa Simba, Luis Miquissone dakika ya 29, likiwa la kwanza kwenye mchezo huo, limemfanya kuweka rekodi ya kufunga bao kwenye mechi zote tatu ambazo Simba imecheza nyumbani, Dar es Salaam kwenye hatua za makundi.

Alifunga bao Simba ikicheza dhidi ya Al Ahly, timu yake ikifunga bao pekee, Februari 23, na bao lingine Machi 16, mwaka huu Simba ikiichapa Al-Merrikh mabao 3-0.

### #4. CHAMA MUUAJI TENA WA AS VITA

Utakumbuka Machi 16, 2019, Simba ilipoifunga AS Vita, Clatous Chama ndiye aliyefunga bao dakika za mwisho zilizoifanya timu hiyo kushinda mabao 2-1 na kutinga robo fainali. Ni Chama huyo huyo aliyefunga bao la pili kwenye mechi ya juzi Jumamosi kwenye goli lile lile la Kusini.

Safari hii akifunga dakika za mwisho za kipindi cha kwanza na kuanza kurahisisha safari ya Simba kwenye robo fainali, kabla ya kutoa pasi kwenye bao la tatu kipindi cha pili na kufunga mwenyewe dakika sita kabla ya mechi kumalizika. Chama amekuwa ndiye muuaji tena kwa mara nyingine wa timu ya AS Vita.

### #5. Wafungaji mabao wote wa**GENI**

Licha ya mabao yote ya Simba kufungwa na wachezaji wa kigeni, lakini nao wote hawakuwa na siku tatu kambini wakitokea kuzichezea timu zao ya taifa. Miquissone aliyefunga bao la kwanza, ndiyo kwanza alikuwa ameshuka kutoka nchini Msumbiji timu yake ikicheza dhidi ya Cape Verde Machi 30.

Chama na Bwalya wao walikuwa wametoka kuichezea timu ya Taifa ya Zambia Machi 29, ikicheza dhidi ya Zimbabwe.

### #6. WACHEZAJI WA AFCON WAIBEBA

Simba imeonekana kubebwa zaidi na wachezaji wengi ambao walikwenda kuzichezea timu zao za taifa kwenye michuano ya kusaka tiketi kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) yanayotarajiwa kuchezwa mwakani nchini Cameroon.

Timu hiyo ilikuwa na wachezaji wengi ambao walitoka kucheza mechi za kufuzu, wengine wakiwa hawana hata siku mbili tangu warejee.

Kwa wachezaji wa Tanzania walikuwa ni Aishi Manula, Shomari Kapombe, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr', na Jonas Mkude ambao walianza kwenye mechi hiyo ya juzi.

Kwa upande wa wachezaji wa kigeni ni Thadeo Lwanga aliyetoka kuichezea timu ya Taifa ya Uganda, Chama timu ya Taifa ya Zambia, na Joash Onyango ambaye alitoka kuichezea timu ya taifa ya Kenya, Harambee Stars.

Hata walioingia, Erasto Nyoni na Hassan Dilunga, walitoka kuichezea Taifa Stars, Meddie Kagere akitoka kuitumikia timu ya Taifa ya Rwanda.

## JE, WAJUA?



TANGU mwaka 1976, Simba imepoteza mechi saba tu ikiwa uwanja wa nyumbani, ambapo mwaka huo ilikubali kipigo cha 1-0 dhidi ya Green Buffaloes ya Zambia, kisha 1978 ikalala 1-0 dhidi AS Vita, 1979 ikachapwa 4-0 na Mufulira Wanderers (Zambia), 1980 ikalambwa 1-0 na Union Douala (Cameroon), 1995 ikapigwa 2-1 na ASEC Mimosas (Ivory Coast), 2008 ikatandikwa 3-1 na Enyimba (Nigeria) na mwaka 2013 ndiyo ukawa mwisho wa kufungwa nyumbani ilipochapwa bao 1-0 na Libolo ya Angola.



Askofu wa Dayosisi ya Central Tanganyika Kanisa Kuu la Angalikana, Dk. Dickson Chilongani (kulia aliyeshika fimbo ya uaskofu) akifurahia jambo na wasaidizi wake ambao ni wachungaji baada ya kumalizika kwa ibada ya Sikukuu ya Pasaka iliyofanyika Dodoma jana. Kutoka kulia wa nne ni Balozi wa Tanzania nchini Zimbabwe, Dk. Emmanuel Mbenah. **PICHA PETER MKWAVILA**

# OSHA yaipa tuzo Kamati ya Bunge Katiba na Sheria

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), umetoa tuzo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kutokana na kutambua mchango wake wa kuboresha utendaji wa wakala hiyo.

Akikabidhi tuzo hiyo mwishoni mwa wiki, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema ushauri wa kamati hiyo umeiwezesha kutengeneza mifumo ya kimtandao ya kurahisisha utendaji wa wakala hiyo.

Pia, kupunguza tozo saba zilizokuwa kero kwa wadau wa OSHA pamoja kuongeza mapato ya wakala hiyo.

"Mara nyingi tumezoea serikali kupewa tuzo kwa kufanya vizuri, lakini tumekuwa tukisahau kuwa kuna baadhi ya walioisaidia serikali kufanya vizuri.

"Tumepima utekelezaji na utendaji wa OSHA katika kuzingatia ushauri wenu, tumeona kwa sasa hata gawio limeendelea kuongezeka linalotolewa na OSHA kwenye serikali, mifumo ya kimtandao imetengenezwa ya kurahisisha utendaji, lakini pia tozo saba zimefutwa, hivyo hatunabudi kuwashukuru kwa mchango huo umeiboresha OSHA," alisema.

Alisema tozo saba ambazo OSHA tayari imezifuta ni ushauri uliotolewa na kamati hiyo.

Alitaja tozo hizo ni pamoja na usajili wa maeneo ya kazi, tozo ya fomu ya usajili, tozo ya ada ya leseni ya kukidhi matakwa ya sheria ya usalama na afya mahali pa kazi.

"Tozo ya ushauri wa mambo usalama na afya, faini zinazohusiana na vifaa vya kuzimia moto, tozo ya elimu kwa umma, tozo ya uchunguzi wa ajali ambayo imepunguzwa kutoka Sh. 500,000 hadi Sh.120, 000.

Nao, wajumbe wa kamati hiyo walisema kuwa kamati hiyo imekuwa ikitoa ushauri kwa OSHA wa namna ya kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu pamoja na kuongeza kipato.

# TASAF yashauri usimamizi kilimo korosho

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

OFISA Malalamiko wa Idara ya Mawasiliano wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF), Makwinja Dismas, amewaomba maofisa ugani wa Wilaya ya Chamwino kusimamia mradi wa kilimo cha korosho unaoendeshwa na wanufaika wa TASAF ili uwe na tija.

Makwinja aliyasema hayo alipokuwa akikagua shamba la korosho linaloendeshwa na kikundi cha wanufaika wa mpango huo lililopo Kijiji cha Mlowa, wilayani humo.

Alisema kilimo hicho kinahitaji usimamizi wa karibu ili kuwa chenye manufaa kwao.

"Kilimo cha korosho ni kigeni mkoani Dodoma hivyo maofisa ugani ambao ni wasimamizi wa wanufaika wa TASAF muwasimamie watu hawa ili mradi wa kilimo hiki cha korosho usonge mbele na kuleta matunda," alisema Dismas.

Alisema miti ya korosho iliyopandwa katika shamba hilo la kikundi inahitaji usimamizi wa hali ya juu wa wataalamu ili kuvuna korosho nyingi.

Alisema ipo haja ya kwenda kutoa utaalam wa kilimo hicho kwa walengwa kwa kuwa wameanzisha shamba hilo kwa fedha wanazopewa na TASAF ili kujikwamua kiuchumi.

Alisema mradi huo ukisimamia vizuri utawasaidia wanufaika kuwa na mradi endelevu na wenye manufaa kwao.

Naye, Mratibu wa zao la korosho wa wilayani humo, Hosea Ndui, alisema wanatoa elimu ya uendeshaji wa kilimo na ufugaji kwa walengwa ili wananchi wajikwamue kiuchumi.

Alisema wanufaika hao wamebuni mradi endelevu na miti ya korosho ikitunzwa kwa kufuata utaratibu shambani hutoa mazao mengi msimu wa mavuno.

"Sisi kama wasimamizi tupo mstari wa mbele kuhakikisha fedha za wanufaika wa mpango huu hazipotei bure badala yake zionyeshe matunda ambayo yatawasaidia wao na familia zao hapo baadae," alisema.

Mnufaika wa TASAF, Yohana Magomba, alisema wameamua kufanya kilimo hicho kwa sababu ni endelevu na kinamanufaa makubwa msimu wa mavuno.

"Kilimo hiki ni kigeni kwetu, lakini tunakimudu kwa sababu tunapata mwongozo kutoka kwa maofisa kilimo," alisema Magomba.

# Wamshukuru Majaliwa ujenzi msikiti wa Ghadafi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAUMINI wa dini ya Kiislamu mkoani Dodoma wamemshukuru Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kwa kuchangia ukarabati wa ujenzi msikiti wa Ghadafi unaotarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. milioni 100.

Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu, alisema Waziri Mkuu ameonyesha moyo wake wa utoaji ili ukarabati huo uwakomboe Watanzania kuiga mfano huo wa kumtolea Mungu.

Kwa upande wake, Katibu wa kamati ya ukarabati wa msikiti huo, Khamis Ally, alimshukuru Majaliwa kwa kuunga mkono kufanikisha ukarabati huo ambao hadi kukamilika unatagharimu zaidi Sh. milioni 100, kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbalimbali ikiwamo rangi, matengenezo ya paa na maeneo ya mifumo ya majisafi na taka.

Ally alisema pamoja na misaada wanayoipata kwa ajili ya ukarabati huo pia waumini wa msikiti huo wamekuwa wakichanga kwa kupitia sadaka zao.

"Kila baada ya sala tumekuwa tukikumbushwa na kuzitoa ili zoezi hili likamilike kwa haraka," alisema.

Hata hivyo, Katibu huyo alisema kuwa mpango uliopo wa ukarabati huo wa msikiti ni pamoja na kuhakikisha unakuwa na uwekezaji wa vitega uchumi kwa kuweka fremu za maduka yatakayojengwa kwenye uzio wa msikiti huo.

Alisema pamoja na kuwapo kwa vitega uchumi vingine kama vile kituo cha ufundi stadi, kozi ya kompyuta, kituo cha elimu ya lugha ya kiarabu na kituo cha afya ikiwamo bweni la wanafunzi, msikiti huo malengo yake ni kuhakikisha unajiendesha wenyewe kiuchumi.



## Mbalizi wataka mji kupangwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wakazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kupanga mji huo mapema ili kuepuka makazi holela yanayoendelea kujengwa na wananchi ili kuepuka gharama kubwa ya kulipa fidia baadaye.

Wananchi hao walisema mji huo unakua kwa kasi, huku kila mwananchi akijenga nyumba yake kulingana na eneo lake huku baadhi ya maeneo yakiwa hayana miundombinu ya barabara za mitaani.

Julius Shila, mkazi wa Mapelele katika Kata ya Nsalala, alisema maeneo mengi ya Mji huo yamepangwa ovyo na haijawahi kutokea eneo lolote likapimwa na serikali zaidi ya wenye mashamba kuuza viwanja kienyeji.

Alisema wana uzoefu wa kuona katika miji mingine inapotakiwa kupangwa upya wananchi wanatakiwa kulipwa fidia za nyumba zao endapo itabainika kuwa miundombinu kama barabara inatakiwa kupita kwenye makazi yao.

"Sasa hivi eneo lililobaki wazi ni la kuelekea Nsalala ambako pia watu wanajenga kwa kasi kubwa sana, ambacho kingefanyika ni serikali kuyawahi maeneo hayo ambayo kwa sasa yako wazi iyapime na watu wamilikishwe vinginevyo itakuwa kama ilivyo Mapelele," alisema Shila.

Alisema kutokana na mpangilio mbaya wa makazi katika Mji huo, hata maeneo ya umma yameanza kuvamiwa zikiwamo Shule na maeneo ya wazi.

Naye Sophia Samson alisema kuna baadhi ya maeneo ya Mji huo ikitokea msiba wanapata shida ya kusafirisha maiti kutokana na kutokuwapo kwa barabara za mitaa.

Alisema wakati wa kuupanga Mji wa Tunduma ulioko katika Halmashauri ya Momba mkoani Songwe, nyumba za watu zilibomolewa na wengine walikuwa wanadai fidia hali ambayo alidai kuwa huwa inachelewesha maendeleo.

Alisema ili kuepuka matatizo ya aina hiyo ni vema serikali ikawa inawahi kupima na kuhakikisha kila mtu anayejenga nyumba eneo lake limepimwa.

"Kinachofanyika sasa hivi ni kila mwenye shamba kugawa viwanja na kuanza kuuza kienyeji, serikali za mitaa huwa zinashiriki kwa sababu viongozi wanachukua asilimia 10 ya kila kiwanja kinachouzwa, sasa unajiuliza wanakubali vipi kuuzwa kwa viwanja eneo ambalo halijapimwa?" alihoji Sophia.

Alisema wakati mwingine baadhi ya wananchi huwa wanagoma kubomolewa nyumba zao huku akitolea mfano wa maeneo ya Kyela wakati wa Ujenzi wa barabara ya Ipinda-Matema, eneo la Inyala katika Halmashauri ya Mbeya wakati wa ujenzi wa barabara ya Simambwe-Inyala na Tunduma.



Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Kikuba, Kata ya Lufilyo, Halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya, wakivuka Mto Mwalisi kwa kushikana mikono kutokana na eneo hilo kutokuwa na daraja na kuleta athari hasa kipindi cha mvua. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Askofu ataka kibano mahubiri yanayopotosha

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeombwa kuwadhibiti baadhi ya wahubiri wanaofanya mahubiri yanayopotosha na mengine yanayodhalilisha utu wa watu, wakiwamo wanaolazimisha kuwapaka mafuta mwili mzima waumini wao wakiwa wamevulia nguo.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Askofu Mkuu wa Kanisa la Moravian Tanzania Jimbo la Kusini Magharibi, Dk. Alinikisa Cheyo, alipokuwa anaongoza ibada ya Ijumaa Kuu katika kanisa hilo Usharika wa Iwambi jijini Mbeya. Alisema baadhi ya wahubiri wamekuwa wakiwadanganya waumini wao kwa kuwapatia vitu kama maji, mafuta, keki na chumvi wakiwaaminisha kuwa vitu hivyo vimetakaswa na vinaponya maradhi mbalimbali.

"Nilipata taarifa kwamba kuna mhubiri mmoja alikuwa anawapaka waumini wake mafuta mwili mzima, walikuwa wanapanga msululu nyumbani kwake kwenda kupata huduma hiyo, sasa unajiuliza kwamba wanapopakwa hayo mafuta wanapakwa wakiwa wamevaa nguo?" alihoji Askofu Cheyo. Pia, alisema kuna mhubiri alikuwa anawauzia waumini wake keki akiwaaminisha kuwa inaponya maradhi mbalimbali, lakini baada ya waumini hao kula walianza kuharisha na kutapika.

Alisema wakati mwingine serikali huwa inachelewa kudhibiti vitendo vya aina hiyo ambavyo vinapotosha wananchi akidai kuwa wananchi huwa hawaelewi haraka na hivyo ni rahisi kudhurika. Aliwataka Watanzania kutokuwa wepesi wa kuamini kila wanachoambiwa na wahubiri hao akidai kuwa kufanya hivyo ni 'ushamba' wa imani na hivyo akawataka kuchuja kila jambo wanaloambiwa ili wasidhurike.

Kwa upande wake Mchungaji wa Kanisa la Moravian Usharika wa Iwambi, Anthony Ntove, aliwataka wakristo kuendelea kuadhimisha sikukuu ya Pasaka kwa kutenda matendo mema yanayompendeza Mungu.

Kuteswa, kufa na kufufuka kwa Yesu kunaashiria ushindi na hivyo akawataka pia kuendelea kuwaombea viongozi mbalimbali wa serikali akiwemo Rais, Samia Suluhu Hassan ili aliongoze taifa kwa mafanikio kama alivyofanya mtangulizi wake Hayati Dk. John Magufuli.

Alisema yeye binafsi ana imani kubwa na rais Samia kuwa ataliongoza vyema taifa huku akidai kuwa ameshaanza kuonyesha uwezo ndani ya siku chache alizoongoza kwa kutoa matamko yenye kuleta matumaini kwa wananchi. "Rais yuko vizuri ila tunaomba wasaidizi wake wasimuangushe, lakini pia ni jukumu letu viongozi wa dini na waumini wetu kuendelea kuwaombea viongozi wetu hawa ili walifikishe taifa letu pale linapostahili," alisema Mchungaji Ntove. Nao baadhi ya waumini wa kanisa hilo waliohudhuria ibada hiyo walisema wana imani kuwa Rais Samia atawafuta vizuri machozi ambayo wanayo baada ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli.

Mmoja wa waumini hao, Eston Kamwela, alisema baada ya kifo cha Dk. Magufuli wengi walikata tamaa wakiamini kuwa taifa lingeyumba lakini ndani ya siku chache za uongozi wa Rais Samia, wameanza kupata matumaini mapya. Sherehe za Pasaka huwa zinafanyika kila mwaka kwa wakristo duniani kote kuadhimisha mateso, kifo na ufufuo wa Yesu Kristo zaidi ya miaka 2000 iliyopita.

# Ukosefu wa daraja watishia wanakijiji

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

ZAIDI ya wakazi 3,000 wa Kijiji cha Kikuba Kata ya Lufilyo Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe wanalazimika kuhatarisha maisha yao kwa kuvuka kwenye maji ya Mto Mwalisi wanapoenda kufuata huduma za kijamii kwenye Makao makuu ya Kata hiyo kutokana na eneo hilo kutokuwa na daraja.

Wakizungumza na wandishi wa habari mwishoni mwa wiki, wananchi wa kijiji hicho walisema wenzao watatu wamepoteza maisha katika vipindi tofauti kwa kusombwa na maji wakivuka mto huo hasa kipindi cha mvua.

Kutokana na hali hiyo, waliiomba Serikali kuwajengea daraja la kudumu ili kuwaondolea tatizo hilo la kuhatarisha maisha yao kwa kuvuka kwenye maji na kusombwa.

Mmoja wa wananchi hao, Rahabu Mwaijande alisema wanatumia muda mwingi kuwasindikiza watoto shuleni na kwenda kuwachukua wakihofia kusombwa na mto huo hali ambayo imekuwa ikiwafanya wasifanye shughuli za kiuchumi.

"Tunamwomba Rais wetu Samia, asikie kilio chetu wananchi wa Kata ya Lufilyo, hapa watu huwa wanatumbukia kwenye mto na wanakufa, tunaomba hapa watujengee daraja la kudumu ili tusihangaike," alisema Rahabu. Naye Rehema Stanslous alisema tatizo la daraja kwenye eneo hilo ni la siku nyingi na viongozi wa kisiasa wamekuwa wakiahidi kulitatua, lakini mpaka sasa hakuna utekelezaji na kwamba baadhi ya watu wamekuwa wakisombwa na maji lakini wanaokolewa.

Alisema awali daraja lilikuwapo katika eneo hilo lakini lilisombwa na maji na hivyo kuwafanya wawe wanavuka chini hali ambayo inahatarisha maisha yao kutokana na mto huo kuwa na maji mengi ambayo yanapita kwa kasi. Alisema kwa sasa katika Kijiji hicho hakuna chombo chochote cha usafiri ambacho kinatumika hasa kipindi cha mvua na kwamba wakati wa kiangazi pikipiki za kubeba abiria maarufu kwa jina la Bodaboda huwa zinavuka.

Mzee Kawoneka Mahenge ambaye pia ni mkazi wa Kijiji hicho alisema wamekuwa wakijenga madaraja ya muda kwa kutumia miti, lakini yanasombwa na mafuriko na hivyo kusababisha warudi tena kwenye kuvuka maji.

Diwani wa Kata ya Lufilyo, Lucas Mwamafupa, alisema daraja hilo ni kiunganishi muhimu kwa wakazi wa Kijiji cha Kikuba ambao wako zaidi ya 3,000 na makao makuu ya Kata hiyo ambako ndiko huduma za kijamii zinakopatikana.

Alisema mbali na huduma ya elimu ambayo watoto wa kijiji hicho wanavuka kwenda kuitafuta, pia huduma zingine kama za Hospitali na soko huwa zinapatikana kwenye makao makuu ya kata.

Aliiomba Serikali iwasaidie kujenga daraja la kudumu kwa maelezo kuwa makao makuu ya Kata hiyo yapo katika Kijiji cha Kipapa na hivyo ili wafike huko ni lazima wavuke mto Mwalisi.

Akizungumza na Nipashe kuhusu tatizo hilo, Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) wa Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Gerard Matindi, alisema tayari ofisi yake imeshapokea malalamiko ya wananchi hao.

Alisema tayari wameshaliingiza daraja hilo kwenye mipango na kwamba kwa sasa wanachosubiri ni fedha, huku akidai kuwa zitakapopatikana wataanza kujenga. Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe ni miongoni mwa halmashauri mkoani Mbeya ambazo miundombinu ya barabara na madaraja imekuwa ikiharibika mara kwa mara kutokana na mvua kunyesha kwa muda mrefu.



# Nkuya aahidi kusimamia vyema majukumu yake

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya Salum, amesema ofisi yake itasimamia vyema majukumu yake ili kuhakikisha masuala yote ikiwamo ya kimazingira yanakuwa salama na hayaathiriwi.

Alisema hayo jana wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa programu za ofisi yake kwa kipindi cha miezi mitatu Januari na Machi 2021, aliyoiwasilisha kwa kamati inayosimamia ofisi za viongozi wakuu wa kitaifa ya Baraza la Wawakilishi.

Dk Saada alisema Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais malengo yake ni kuhakikisha inakuwa na mfumo bora wa kisera na kisheria kwa taasisi inazozisimamia

Pia, alisema kupitwa na muda kwa baadhi ya sera na sheria zinazosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni changamoto ambayo tayari imeanza kufanyiwa kazi na kutoa mapendekezo ya kurekebisha Sera na Sheria hizo kwa ajili ya utekelezaji ili kuendana na kasi ya kiutendaji kwa mujibu wa taratibu.

"Rasimu ya Sera ya Dawa za kulevya imeandaliwa na ipo katika hatua ya kuwasilishwa Baraza la Mapinduzi. Rasimu ya Sera ya Mazingira ipo katika hatua ya maandalizi na rasimu ya marekebisho ya Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ipo katika hatua ya kupelekwa kwa wadau," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Kamati inayosimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi, Hassan Khamis Hafidh, aliyomba Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kusimamia vyema majukumu yao ili Zanzibar iendelee kuwa salama kwa masuala wanayoyaratibu.

Hassan alisema Zanzibar inahitaji kuwa salama kulinda na kuhifadhi mazingira, kutokubali kuwa sehemu ya wapitishaji na wauzaji na wasambazaji dawa za kulevya, kuzingatia vyema masuala ya upatikanaji wa haki za watu wenye ulemavu na kuwa na jamii isiyokuwa na maambukizi ya virusi vya Ukimwi. Aliwataka viongozi wa ofisi hiyo kuhakikisha matumizi na mapato yanaendana na utekelezaji wa mpango wa bajeti. Akitoa maelezo ya mradi wa kujenga uwezo wa kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa maeneo ya pwani katika eneo la Kilimani, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Khadija Khamis Rajab, alisema mafaniko makubwa yamepatikana katika mradi huo na hifadhi ya fukwe imerudi ikilinganishwa na awali maji yalikuwa yakiingia karibu na maeneo ya makazi ya wananchi.

Mradi huo ambao umefadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa kimazingira ulianza 2013 - 2018 na shughuli zilizofanyika katika kurudisha mazingira ni upandaji wa miti ya mikoko na kuweka ukuta kwa kutumia mawe kwa ajili ya kuzuia maji ya bahari yasipande juu na kuathiri maeneo ya makazi.

Katibu wa jumuiya inayosimamia mazingira ZACEDY kupitia eneo la mradi wa kujenga uwezo wa kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa maeneo ya pwani katika eneo la Kilimani, Jamal Khamis Juma, alisema kwa kiasi kikubwa wamefanikiwa kurudisha eneo hilo kwa kushirikiana na Ofisi ya Wilaya Mjini na wanajamii



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman, akilikagua Soko la Samaki lililopo katika Kijiji cha Njuguni Jimbo la Wingwi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wachuuzi watakiwa kulitumia vizuri soko jipya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amewataka wananchi na wachuuzi wa samaki wa Kijiji cha Njuguni, Jimbo la Wingwi Pemba kulitumia soko jipya la kisasa la samaki lililojengwa na serikali ili kukidhi mahitaji yao ya biashara.

Alisema kitendo cha wachuuzi wa samaki wa kijiji hicho kuendelea kuuza samaki wao kando ya barabara, kinahatarisha maisha yao na kinaweza kuleta athari ya afya zao kutokana na vumbi linalosababishwa na magari yanayopita kila wakati eneo hilo.

Akiendelea na ziara yake huko Kisiwani Pemba kukagua miradi ya maendeleo na kujuachangamoto zinazowakabili wananchi, alisema ujenzi wa soko hilo umezingatia matakwa yao ambayo wanapaswa kuyasimamia.

Alisema haipendezi hata kidogo kuona serikali inajenga na kuimarisha miradi ya maendeleo iliyobuniwa na wananchi wenyewe akitoa mfano soko hilo na baadaye wananchi hao kushindwa kulitumia. Aliwaambia wananchi na wachuuzi wa samaki wa Njuguni kwamba huduma bora ndizo zinazotoa fursa kwa mteja kuzifuatilia mahali popote bila ya kujali umbali wa bidhaa iliyopo.

Hemed alisema katika kukabiliana na changamoto inayowakabili wananchi wa jimbo hilo na wale wa vijiji jirani ameuagiza uongozi wa Wilaya ya Micheweni kupitia halmashauri ya wilaya hiyo kutafuta eneo jipya litakalojengwa soko kubwa litakalokidhi mahitaji yote kwa kuzingatia miundombinu na jografia halisi.

"Wananchi wa Wingwi ni vyema wakafunuka na kuanza kulitumia soko lao huku serikali kuu kupitia uongozi wa Wilaya na Halmashauri ya Micheweni pamoja na viongozi wa jimbo itabeba dhima ya kuwapatia majokofu kwa lengo la kuhifadhi samaki wao," alisema. Aliwahakikishia wachuuzi hao kuwa soko la samaki halichelewi kuzoeleka kwa kupata wateja kutokana na huduma kuwa muhimu katika maisha ya kila siku ya mwanadamu.

Akizungumzia kero za huduma za majisafi na salama, umeme, afya na miundombinu ya barabara inayowakabili wananchi wa vijiji vya Mkia wa Ng'ombe na Chanja Kipange, huko Kisiwani Pemba, Hemed aliahidi kwamba huduma hizo muhimu zitafikishwa katika maeneo yao ili kuwaondolea dhiki inayowakabili.

Kuhusu miradi ya ujasiriamali ya uchimbaji wa mawe kwa ajili ya kokoto inayofanywa na wananchi wa Kijiji cha Mjini Wingwi, alisema serikali haiwezi kuruhusu uendelezaji wa mradi huo kwa vile umeshaleta athari na kusababisha kupotea kwa maisha ya wananchi.

Alisema katika njia ya kutafuta mbadala wa masuala ya ajira katika kijiji hicho, zipo sekta za uvuvi na kilimo pamoja na ujasiriamali kupitia vikundi vya ushirika ambavyo wanachi hao wanavitumia kuendesha maisha yao.

Akitoa taarifa ya utekelezaji kazi za maendeleo wa Wilaya ya Micheweni, kwa mwezi Novemba, mwaka 2020 hadi Machi 2021, Mkuu wa wilaya hiyo Mohd Seif, alisema halmashauri ya wilaya hiyo imejipangia kukusanya mapato zaidi ya Sh. milioni 149.

Alisema kutokana na ushirikiano mkubwa wa watendaji na viongozi wake wamefanikiwa kukusanya zaidi ya Sh. milioni 194 na kuvuka lengo walilojipangia.

Wakati huo huo, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar alipata fursa ya kulitembelea eneo la Bandari ya Micheweni lililowekwa kufungua fursa za uwekezaji wa wawekezaji wazawa na wageni chini ya usimamizi wa Rais wa Zanzibar aliyelenga kuweka mikakati maalum ya uwekezaji katika kisiwa cha Pemba.

Akitoa ufafanuzi wa harakati za uimarishaji wa eneo hilo, Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Kahtibu, alisema taasisi zote zinazohusika na uhuishaji wa miundombinu ya eneo hilo zinaendelea vyema na majukumu yake.

# 'Elimu itolewe wanafunzi wanaojifungua kurudi shule'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amewataka wakurugenzi na wakuu wa vitengo vya wizara hiyo kutoa elimu kwa jamii ya kuwarudisha shule wanafunzi waliojifungua baada ya kupata ujauzito wakiwa shuleni.

Akizungumza jana katika kikao cha kupokea ripoti ya tathmini ya utekelezaji wa sera ya wanafunzi kuendelea na masomo baada kujifungua (re-entry policy) kilichofanyika mjini Unguja, alisema viongozi wa wizara hiyo wanawajibu wa kutoa elimu hiyo katika maeneo yote yaliowazunguka.

Aliitaka jamii kuacha tabia ya kuwabeza watoto wanaopata ujauzito wakiwa bado hawajamaliza masomo, kwa sababu nao wana malengo ya kuwa wataalamu wazalendo katika taifa lao.

Alisema wazazi nao wanapaswa kuachana na mila za kuwaozesha watoto mapema baada ya kupata ujauzito na kuacha tabia ya kumtenga na kuwa mstari wa mbele kutetea haki zao ili warudi katika masomo wakiwa na lengo la kutimiza ndoto zao.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Ali Khamis Ali, alisema pamoja na kuja na wazo hilo la kutaka kuwarejesha wanafunzi shule baada ya kujifungua, lakini ni vyema kutafuta njia za kudhibiti kutopata mimba watoto ili kuwa na taifa imara.

Alisema sio watoto wote wanaopata ujauzito wakiwa shule wanakubali kurejea baada ya kujifungua kutokana na sababu mbalimbali na taifa inapoteza wanafunzi wengi wenye uwezo na vipaji vizuri kwa maendeleo ya nchi.

Aliwataka washiriki wa kikao hicho kutoa mitazamo itakayosaidia kupata njia rafiki na nyepesi za kuwarejesha wanafunzi shule baada ya kujifungua pamoja na hizo mbinu za kudhibiti mimba kwa wanafunzi.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu Sayansi na Utamaduni (UNESCO), Tirso Dossantos, alisema shirika hilo litaendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuhakikisha wanawasaidia vijana kupata haki yao ya elimu ya lazima.

Alisema anaamini kikao hicho kitasaidia kupatikana njia mbadala za kuwasaidia watoto wanaopata mimba wakiwa shuleni kurudi kuendelea na masomo bila ya kuwapo changamoto yoyote.

Kwa upande wake mwasilishaji wa ripoti ya tathmini ya utekelezaji wa sera ya wanafunzi kuendelea na masomo baada ya kujifungua, Mshauri Abdullah Khamis, alisema takwimu zinaonyesha kuwa wanafunzi wengine wanaopata ujauzito huogopa kurudi shule kutokana na kunyanyapaliwa katika jamii na hata shule.

Alisema utayari wa wazee wa kuwashauri vizuri watoto wao katika kipindi cha ujauzito utawasaidia waathirika hao kurudi shule ili kuvitumia vipaji vyao na kutumiza malengo yao.

HABARI KIMATAIFA

## Matumizi mto Nile yajadiliwa DRC

**Kinshasa,** DRC

MAZUNGUMZO ya siku tatu kutafuta mwafaka wa matumizi ya maji ya Mto Nile yameanza jijini Kinshasa mwishoni mwa wiki, nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Mawaziri wa Mambo ya nje kutoka Misri, Ethiopia na Sudan walikutana katika kikao hicho ambacho kiliongozwa na Rais Felix Thisekedi, ambaye pia ni Mwenyekiti wa mataifa ya Umoja wa Afrika (AU).

Kitovu cha mzozo wa matumizi ya maji hayo, ni hatua ya Ethiopia tangu mwaka 2011 kuanza ujenzi wa bwawa kubwa la kuzalisha umeme na kutumia maji ya mto huo.

Misri na Sudan zilisema kitendo hicho cha Ethiopia kitasababisha raia wake kukosa maji huku Misri ikisisitiza kuwa ni chanzo pekee cha maji kwa watu wake, madai yanayopingwa na Ethiopia.

Rais Tshisekedi alionyesha nia ya kupata suluhu kati ya nchi hizo, aliwahi kutembelea Misri na Ethiopia Februari na kuahidi kupatanisha pande zote zinazokinzana.

Mara ya mwisho kuwapo kwa mazungumzo kama hayo, ilikuwa Januari chini ya AU, ingawa hakuna mwafaka wowote uliopatikana. **RFI**

## Watu 100 wauawa shambulizi nchini Somalia

**Mogadishu,** SOMALIA

ZAIDI ya watu 100 wameuawa katika mashambulizi yaliyotokea kwenye kambi za jeshi nchini Somalia.

Kundi la kigaidi la Al-Shabaab, lilithibitisha kuhusika.

Magari mawili yaliyotegwa mabomu yaliripuka kwenye vituo viwili vya kijeshi kwenye Wilaya ya Awdhegle na Kijiji cha Bariire kwenye jimbo tete la Shabelle.

Kisha yalifuatia mashambulizi makali kutoka kwa wanamgambo wenye silaha waliovamia kambi za jeshi.

Msemaji wa jeshi la Somalia alisema wamefanikiwa kuwadhibiti na kuwauwa wanamgambo 116, ikiwamo makamanda watatu wa kundi la Al Shabaab huku serikali ikipoteza wanajeshi wanne.

Kundi la Al Shabaab lilidai kuhusika na shambulizi hilo, kupitia kituo cha redio cha Andalus likisema, wanajeshi 47 wa serikali wameuawa. **DW**

# Chanjo AstraZeneca yaua 7 Uingereza

**London,** UINGEREZA

WATU saba wamefariki dunia kutokana na damu kuganda, baada ya kupewa chanjo ya Oxford-AstraZeneca, mamlaka ya kudhibiti dawa imeithibitishia BBC.

Kwa ujumla watu 30 kati ya milioni 18 waliopewa chanjo hiyo kufikia Machi 24, mwaka huu wamekabiliwa na hali ya damu kuganda.

Bado haijulikani ikiwa ni bahati mbaya tu au athari ya kweli ya chanjo.

Shirika la Udhibiti wa Dawa na Bidhaa za Afya, lilisema faida ya chanjo zinaendelea kuzidi madhara yake.

Hata hivyo, hali ya kuganda kwa damu kwenye ubongo, kitaalamu 'cerebral venous sinus thrombosis' (CVSTs) zimesababisha nchi nyingine, zikiwamo Ujerumani, Ufaransa na Canada, kudhibiti matumizi wa chanjo hiyo.

**Uchunguzi wa kubaini ikiwa chanjo ya AstraZeneca inasababisha hali isiyokuwa ya kawaida ya damu kuganda mwilini unaendelea.**

Shirika la Afya duniani na Wakala wa Dawa wa Ulaya wanasema faida za chanjo hiyo huzidi hatari zozote.

Takwimu zilizotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa (MHRA) mwishoni mwa wiki, zilionesha kuwa watu 22 walipata CVST ambayo ni aina fulani ya mgando wa damu kwenye ubongo.

Hali hiyo ilielezwa kutokana na viwango vya chini vya seli, zinazosaidia damu kuganda, mwilini.

MHRA pia ilibaini watu wengine nane walikabiliwa na tatizo la damu kuganda mwilini.

MHRA iliithibitishia BBC kupitia barua pepe, kwamba "inasikitika watu saba wamefariki."

Dk. June Raine, Ofisa Mkuu Mtendaji wa MHRA, alisema: "Manufaa ya kudhibiti maambukizi ya Covid-19 na changamoto zake yanaendelea kuwa juu kuliko hatari yoyote kwa hiyo watu walikubali kupewa chanjo walipoombwa kufanya hivyo."

Uchunguzi wa kubaini ikiwa chanjo ya AstraZeneca inasababisha hali isiyokuwa ya kawaida ya damu kuganda mwilini unaendelea.

Shirika la Dawa la Muungano wa Ulaya lilisema halijathibitisha, ingawa kuna uwezekano.

Kumeshuhudiwa visa viwili vya damu kuganda kwenye ubongo (CVST) baada ya watu kutumia chanjo ya Pfizer nchini Uingereza, kati ya watu zaidi ya milioni 10 waliochanjwa hawakuwa na viwango vya chini vya seli ya inayosaidia damu kuganda. **BBC**



Papa Francis akionyesha ishara ya njia ya msalaba katika Misa ya Sikukuu ya Pasaka katika Kanisa la St. Peter Basilica mjini Vatican. Jana, mamilioni ya waumini wa dini ya Kikristo duniani walisherehekea sikukuu hiyo. **PICHA: DW**

# Vifo mafuriko vyafikia 44

**INDONESIA**

TAKRIBANI watu 44 wamefariki dunia baada ya mafuriko na maporomoko ya udongo, yaliyokikumba kisiwa kilichopo Mashariki mwa Indonesia.

Waokoaji na maofisa wa serikali walisema, inawezekana idadi ya vifo ikaongezeka.

"Kuna watu 44 pamoja na tisa wamejeruhiwa na wengi bado wapo kwenye tope," Msemaji wa Wakala wa Taifa wa Kudhibiti Maafa, Raditya Jati, aliliambia Shirika la Habari la AFP.

Saa chache kabla ya watu kuamka na kusheherekea sikukuu ya Pasaka, mvua ilianza kunyesha katika kisiwa kilicho na wakatoliki wengi cha Flores.

Taarifa zilisema matope yaliingia kwenye makazi ya watu huku madaraja na barabara katika kisiwa hicho vikiharibiwa.

Waokoaji waliendelea na shughuli ya uokoaji huku kikwazo kikiwa kuyafikia maeneo hayo kutokana na mvua na mawimbi ya bahari. Awali taarifa za mamlaka zilisema vifo vilikuwa 23.

"Bado tunakusanya taarifa za idadi ya watu waliojeruhiwa na kwamba hali mbaya ya hewa inatarajiwa kwa wiki nzima," alisema msemaji huyo.


Aidha mafuriko katika mji wa Bima, siku hiyo ya jana pia, yalisababisha vifo vya watu wawili, Kaskazini mwa Nusa Tenggara, kulingana na taarifa ya wakala wa maafa na kwamba wilaya nne zilifurika.

Pia Januari mwaka huu, nchini humo, watu 40 walifariki katika mji wa Sumedang uliopo Mashariki mwa Java huku Septemba mwaka jana karibu watu 11 walikufa eneo la Borneo na 12 wakipoteza maisha miezi michache iliyopita, Sulawesi.

Sababu ya kutokea mafuriko na maporomoko ya udongo Indonesia kunatajwa kuchochewa na ukataji miti ovyo, kulinga na wana mazingira.

Wakala wa maafa, ulikadiria kuwa Waindonesia milioni 125 karibu nusu ya idadi ya watu wote nchini humo, wanaishi kwenye maeneo ya hatari ya kukumbukwa na maporomoko ya udongo. **DAILY MONITOR**

## HABARI MICHEZO



# LUKAKU ASIFU UAMUZI SAHIHI KUTUA INTER MILAN

**MILAN,** Italia

ROMELU Lukaku amesema ana "wakati bora" baada ya kufikisha mabao 20 kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa mara ya pili mfululizo, huku akielezea kuwa alifanya uamuzi sahihi kujiunga na Inter.

Aliwahi mpira wa kichwa alioupiga na kugonga mwamba, lakini baadaye alikaa vizuri na kuumalizia na kuifungia Inter bao pekee kwenye mchezo huo dhidi ya Bologna, Jumamosi.

Ushindi huo umeifanya Inter kupaa kileleni kwa tofauti ya pointi nane dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja AC Milan ambao wapo nafasi ya pili.

Bao hilo la Lukaku limeifanya Inter kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kulibeba taji hilo na kuwa mchezaji wa saba kufunga mabao 20 kwenye misimu miwili mfululizo kwenye ligi katika historia ya klabu hiyo.

"Nina furaha kubwa na ushindi wa leo; ulikuwa mchezo mgumu. Tulihitaji kucheza kwa kujituma zaidi," alisema Lukaku - ambaye alisajiliwa Inter akitokea Manchester United mwaka 2019 - akiiambia televisheni ya Inter.

"Ni wakati bora kwangu - nilifanya uamuzi sahihi kuja hapa.

"Nitafanya kila kitu niwezacho kwa timu kwa sababu mimi si kitu bila ya wachezaji wenzangu.

"Kundi hilo ni muhimu zaidi kuliko kitu chochote. Tuna malengo yetu na tunahitaji kuendelea kuyaweka mbele."

# Pogba atajwa kutimkia Real

**MANCHESTER,** England

HATIMA ya nyota ya kiungo wa Manchester United, Paul Pogba, imeendelea kuwa na kizungumkuti huku akiendelea kuhusishwa zaidi na kuondoka klabuni hapo.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka nchini Hispania, wakala wa Pogba, Mino Raniola, alimhusisha kwenye mazungumzo yake na Real Madrid.

Alhamisi, wakala Raniola alisafiri kuelekea nchini Hispania na kufanya mazungumzo na Rais wa Klabu ya Real Madrid baada ya kukamilisha mazungumzo na klabu ya Barcelona.

Raniola anaaminika kuwa alikuwa na mazungumzo na Barcelona juu ya Erling Haaland, halafu akashuka mji Mkuu wa Hispania kufanya mazungumzo na Real Madrid juu ya Pogba.

Pogba anaendelea kuhusishwa na klabu kadhaa, lakini kwa mujibu wa Calciomercato nyota huyu alitajwa katika maongezi ya Raniola na Florentino Perez, na Madrid wako tayari kukamilisha uhamisho wake.

Mkataba wa nyota huyu mwenye miaka 28 raia wa Ufaransa unaisha mwishoni mwa msimu ujao wa majira ya joto, na hadi sasa amefunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho 'asisti' 30 kwa msimu huu wa 2020-21 chini ya kocha Ole Gunnar Solskjaer.






# Guardiola: Sitausahau msimu huu wa 2020/21

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema "kamwe sitausahau msimu huu" wakati vinara Manchester City wakikaribia kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England baada ya kuibuka na ushindi dhidi ya Leicester City iliyopo nafasi ya tatu, juzi Jumamosi.

Mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Benjamin Mendy na Gabriel Jesus yaliifanya Man City kuhitahi pointi 11 katika mechi saba zilizobaki ili kutwaa taji hilo kwa mara ya tatu ndani ya misimu minne.

"Naipenda Ligi Kuu England kuliko mashindano yoyote. Tumekaribia, tumekaribia sana," aliongeza Guardiola baada ya timu yake kuongoza kwa tofauti ya pointi 17 kileleni.

"Mabingwa ni Liverpool, wana taji - lakini tunakaribia sana kulibeba."

Guardiola amesema City walionyesha jitihada kubwa sana msimu huu huku wakicheza bila mashabiki uwanjani kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

"Watu wakiwa wamefungiwa tulicheza mechi bila mashabiki," alisema. "Kamwe sitausahau msimu huu."

Huo ulikuwa ni mchezo wao wa kwanza tangu watangaze kwamba mfungaji wao wa wakati wote Sergio Aguero ataondoka mwishoni mwa msimu huu.

HABARI MICHEZO

# Aguero ashauriwa kwenda Man United

**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Sergio Aguero, ameambiwa kama anataka kubaki kwenye Ligi Kuu England, basi anapaswa kuhamia kwa wapinzani wao, Manchester United.

Hayo ni maoni ya mshambuliaji wa zamani wa Man United, Dimitar Berbatov ambaye anaamini kama Aguero atatua Old Trafford basi atamaliza tatizo la umaliziaji katika kikosi hicho kinachonolewa na kocha Ole Gunnar Solskjaer.

Aguero mwenye umri wa miaka 32, ataondoka pale kweye dimba la Etihad mwishoni mwa msimu ambapo mkataba wake ndio utakuwa unafikia mwisho.

Man City haina mpango wa kumwongezea mkataba mwingine na Berbatov anaona kwamba, mchezaji huyo atafiti zaidi kama akienda kwenye klabu yake hiyo ya zamani.

“Naamini Aguero atafiti zaidi kucheza Manchester United, pale ndio sehemu sahihi kwake,” alisema Berbatov akinukuliwa na Daily Mail.

Aguero amekuwa akihusishwa na klabu nyingi ambazo zinatajwa kuwania saini yake kama Barcelona, Juventus, PSG na Chelsea.





# IHEANACHO AJIFUNGA UPYA LEICESTER

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Leicester City na timu ya taifa ya Nigeria, Kelechi Iheanacho, amesaini mkataba mpya wa kuendelea kubaki klabuni hapo hadi mwaka 2024.

Akiwa na umri wa miaka 24, Iheanacho yupo kwenye kiwango bora msimu huu na tayari ameshapachika mabao matatu katika michezo minne.

Kiwango chake kimemfanya mshambuliaji huyo apatiwe tuzo ya mchezaji bora wa Machi kwenye Ligi Kuu England.

Tangu ajiunge na Leicester City mwaka 2017 akitokea Manchester City, Iheanacho ameitumikia timu hiyo kwa jumla ya michezo 117 na kuzifumania nyavu mara 32.

“Siwezi kuelezea ninavyojisikia. Nimefurahi sana kwa Leicester City kuniongezea mkataba,” alisema Iheanacho akiiambia BT Sports.

“Ninajisikia vizuri kuwa hapa, imekuwa kama ni familia. Ninafurahi kuwa hapa na ninaimani nitaendelea kuwapo hapa kwa miaka mingi zaidi,” aliongeza.

# *Torreira kutimkia Boca Juniors*

**MADRID,** Hispania

KIUNGO wa Arsenal raia wa Uruguay, Lucas Torreira, amesema anataka kuondoka Ulaya na kwenda kujiunga na Boca Juniors ya Argentina.

Toreira kwa sasa anacheza kwa mkopo kule Atletico Madrid ya Hispania na sasa akili yake ni kutaka kurudi bara la Amerika Kusini kwenda kumalizia soka lake.

Torreira mwenye umri wa miaka 25, amesema amefikia kufanya uamuzi huo baada ya mama yake kupoteza maisha kutokana na corona mapema wiki iliyopita.

“Usiku ambao mama yangu alifariki dunia, nilimwambia mwakilishi wangu kuwa sitaki kucheza Ulaya tena na ninataka kuhamia Boca,” aliandika Torreira kwenye ukurasa wake wa Instagram.

Aidha, kiungo huyo amebainisha kuwa watu wengi wataona uamuzi huo ameufanya kutokana na kuchanganywa na kumpoteza mama yake, lakini zilikuwa ni ndoto zake za miaka mingi kuichezea miamba hiyo ya Argentina.

“Wengi wanaweza kushangaa, lakini kuichezea Boca Juniors ni ndoto yangu kwa muda mrefu sana, hivyo naona huu ndio wakati wake.

“Hata baba yangu nilimuahidi kuwa siku moja nitakwenda kucheza Boca Juniors,” alisema.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAZARD FITI KUIVAA LIVER UEFA KESHO

## Zidane asema ana matumaini ya kumpata yeye na Valverde kwa mchezo huo ambao...

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane anasubiri kuona kama Eden Hazard atakuwa fiti kurudi kwenye kikosi cha Real Madrid kitakachocheza na Liverpool kesho, Jumanne.

**Madrid wataingia dimbani kwenye mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool kabla ya kuivaa Barcelona katika mchezo wa 'Clasico' wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.**

Lakini kocha Zidane ana matumaini kwamba kikosi chake kitaongezewa nguvu dhidi ya 'Wekundu' hao wa Anfield.

Hazard alirudi kwa muda mfupi kutoka majeruhi kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa, lakini baadaye akaumia tena na hakucheza kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atalanta na hakuweza kwenda kuichezea Ubelgiji.

Kocha wa Ubelgiji, Roberto Martinez pia hakuwa na uhakika kama winga huyo aliyenunuliwa kwa euro milioni 100 ataweza kushiriki michuano ya Euro 2020.

Hazard anaweza kurudi dimbani Jumanne, huku Madrid pia wakifikia kumleta Federico Valverde.

"Matumaini yetu tunaweza kuwapata Valverde na Hazard," alisema Zidane akiwaambia waandishi wa habari Jumamosi.

"Tutaona kesho (leo) nini kitakachotokea kama tutaweza kuwa naye.

"Leo haikuwezekana, lakini nina matumaini kwamba, Jumanne anaweza kuwa na sisi kikosini."

Hazard amefunga mabao sita dhidi ya Liverpool katika mechi 16 dhidi ya Chelsea. Lakini amecheza mechi 36 na ameanza 29 kwa Madrid tangu alipojiunga nayo Juni mwaka 2019, akifunga mabao manne na kutoa pasi za mwisho tano katika nafasi 38 alizotengeneza.

## ZISIKUPITE

### MATA KUONGEZA MKATABA

KIUNGO wa Manchester United, Juan Mata, mwenye umri wa miaka 32, anatarajiwa kupewa mkataba mpya wa mwaka mmoja na klabu hiyo. ***(Daily Star Sunday)***

### RABIOT AWINDWA BARCELONA

KIUNGO wa Juventus, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 26, ambaye amekuwa akihusishwa na Everton, anaweza pia kuwaniwa na Barcelona. ***(Calciomercato)***

### HAALAND KUMRITHI AGUERO

ERLING Haaland amekuwa chaguo la kwanza kwenye usajili wa Manchester City inayonolewa na kocha Pep Guardiola, wakati klabu hiyo ikitarajia kumwachia Sergio Aguero, 32, aondoke. ***(Sunday Mirror)***

### ARSENAL KUMUUZA BUKAYO

ARSENAL inaweza kufikiria kumuuza mchezji wake kinda, Bukayo Saka mwenye umri wa miaka 19, ili kutafuta fedha za kumsajili kiungo wa Real Madrid na Norway, Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 22, kwa mkataba wa kudumu. ***(Sunday Times)***

### DE GEA KUACHWA AONDOKE

MANCHESTER United ipo tayari kumuachia golikipa wake, David de Gea mwenye umri wa miaka 30, ambaye ameonyesha wazi kwamba anataka kuondoka hapo Old Trafford kipindi cha majira ya joto kinachokuja. ***(Sunday Mirror)***

### EVERTON YAMTAKA DYBALA

KLABU ya Everton inatarajia kumsajili mshambuliaji wa Juventus na Argentina, Paulo Dybala, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, hayupo tayari kujiunga na 'Toffees' hao. ***(CaughtOffside)***

### HAALAND HATABAKI DORTMUND

MKUU wa soka wa Borussia Dortmund, Sebastian Kehl, emekubali kwamba klabu hiyo itafikia wakati itashindwa kumbakisha straika wao, Erling Braut Haaland, 20, raia wa Norway. ***(Goal)***

### ATLETICO WAMTAKA WINKS

KLABU ya Atletico Madrid inawania kumsajili kiungo wa Tottenham na England, Harry Winks, mwenye umri wa miaka 25, ambaye hapati muda wa kutosha kucheza chini ya kocha, Jose Mourinho. ***(Sky Sports)***

### ICARDI AWANIWA UNITED

STRAIKA wa Paris St-Germain na Argentina, Mauro Icardi, 28, anawaniwa na Manchester United kuwa mrithi wa muda mrefu wa Edinson Cavani, 34. ***(Teamtalk)***

### GUDMUNDSSON AWANIWA CITY

MANCHESTER City inawania kumsajili mlinzi wa kushoto wa FC Groningen, Gabriel Gudmundsson mwenye umri wa miaka 21. ***(TodoFichajes)***

HABARI MICHEZO

## Kocha Mmisri, Mmalawi waomba kuinoa Biashara

**Na Shufaa Lyimo**

JUMLA ya makocha 45 kutoka nchi mbalimbali wametuma wasifu wao (CV) kuomba kuinoa Klabu ya Biashara United, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu jana kutoka Musoma mkoani Mara, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Haji Mtete, alisema mpaka sasa tayari wamepokea CV za makocha 45 ambao wameonyesha nia ya kuinoa timu yao.

Katibu huyo alizitaja nchi ambazo makocha wameonyesha nia ya kuifundisha timu yao kuwa Misri, Rwanda, Uganda, Kenya, Malawi pamoja na Tanzania.

Alisema mwisho wa kupokea maombi hayo ni Aprili 22, mwaka huu na baada ya hapo Kamati ya Utendaji ya klabu hiyo itakutana na kupitia CV hizo, na kisha watatoa taarifa ya kocha aliyelamba dume kuinoa Biashara United.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Selemani Mataso, alisema wanahitaji kocha wa kigeni kwa sababu wanafaida kubwa wanapokabidhiwa timu.

## Simba Queens jicho kwa Alliance Girls

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa timu ya Wanawake ya Simba, Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', amesema kikosi chake kinaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiwinda dhidi ya Alliance Girls wakati huu wakiendelea kusubiri ratiba mpya.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mgosi alisema awali walipaswa kucheza mechi hiyo jijini Mwanza Machi 26, mwaka huu lakini ilishindikana kutokana na msiba wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli.

"Tunaendelea na mazoezi huku tukiwa tunasubiri ratiba ambayo itaonyesha tunakutana lini na wapinzani wetu," alisema Mgosi.

Kuhusu hali za wachezaji, Mgosi alisema wote wanaendelea vizuri na mpaka sasa hana majeruhi hata mmoja.

# MIQUISSONE ACHUNGULIA KIATU CHA DHAHABU CAF

**Na Mwandishi Wetu**

WINGA wa Simba, Luis Miquissone, amebisha hodi katika orodha ya wachezaji wanaowania Kiatu cha Dhahabu kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kuwa miongoni mwa waliopo kileleni kwa kufunga mabao matatu hadi sasa.

Miquissone ambaye juzi alifunga bao la kwanza wakati Simba ikiibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya AS Vita ya DR Congo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, sasa anaungana kileleni mwa orodha ya wafungaji na Mohamed Ali Ben Romdhane wa Esperance ya Tunisia na Ayoub El Kaabi wa Wydad Casablanca ya Morocco, ambao kila mmoja ana mabao matatu.

Mabao mengine ya Miquissone alifunga katika mechi dhidi ya Al Ahly ya Misiri kwenye Uwanja wa Mkapa wakati Simba ikiibuka na ushindi wa bao 1-0, na lingine akifunga dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan wakishinda 3-0 katika uwanja huo.

Wachezaji wengine wa Simba wanaoifukuzia nafasi hiyo kwa karibu ni kiungo Clatous Chama na mshambuliaji Chris Mugalu, ambao kila mmoja amecheka na nyavu mara mbili katika michuano hiyo itakayofikia ukingoni Ijumaa kwenye hatua ya makundi.

Miquissone pia, tayari ameshaingia mara mbili katika kikosi bora cha wiki cha Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini pia bao lake dhidi ya Al Ahly likitangazwa kuwa bao bora la wiki katika wiki ya michuano hiyo.

Kadhalika, Miquissone ambaye ni raia wa Msumbiji, alitangazwa mchezaji bora wa mechi hiyo dhidi ya Al Ahly baada ya kuonyesha kiwango cha hali ya juu katika mchezo huo.

Mabao yake yameisaidia Simba kutinga robo fainali ya michuano hiyo ikiwa kinara wa Kundi A baada ya kufikisha pointi 13, ikizipiku Al Ahly yenye alama nane, DR Congo pointi nne pamoja na Al-Merrikh ambayo inaburuza mkia ikiwa na alama mbili hadi sasa.

Simba itashuka tena dimbani Ijumaa jijini Cairo, Misri dhidi ya Al Ahly, huo ukiwa ni mchezo wa mwisho kukamilisha hatua ya makundi, na baada ya hapo itasubiri droo kujua mpinzani wake kwenye hatua ya robo fainali.

WANGU HUU...



Wachezaji wa timu ya Msimbazi Rover, Shaban Alli (Kulia) na Amani Said, wakiwania mpira wakati wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Msimbazi Center jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Lwanga: Tatizo nguvu zangu si rafu*

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mkabaji wa Simba, Thadeo Lwanga, amesema yeye hachezi rafu kama ambavyo baadhi ya mashabiki ila ana nguvu kitu ambacho kinawashinda wachezaji wengi wa timu pinzani anaokutana nao.

Akizungumza baada ya mechi dhidi AS Vita ya DR Congo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Lwanga alisema mchezo wa mpira wa miguu unatakiwa utumie nguvu pia na hasa namba ambayo anaicheza ya kiungo wa kuzuia haifai kucheza mpira laini.

"Si kweli, mimi sichezi rafu, ila nina nguvu na natumia nguvu inapohitajika, na kama unavyojua namba yangu ninayocheza, ninapashwa kucheza kwa nguvu ili kuzuia mashambulizi ya timu pinzani, inaonekana ninawashinda," alisema mchezaji huyo raia wa Uganda.

Kuhusu mechi dhidi ya AS Vita, Lwanga alisema walicheza kwa mfumo wa kukaa nyuma, lakini wakiupata mpira wanashambulia kwa kasi, ikiwamo kutumia nafasi kama inawezekana na kurejea tena nyuma kuzuia.

"Tumefurahi kutinga hatua ya robo fainali, tulicheza mechi hii kwa umakini sana, tulikuwa tunacheza kwa kuzuia, lakini tukiupata mpira tunashambulia kwa kasi kutafuta mabao na baada ya hapo tunarudi tena kulinda lango letu na imetusaidia," alisema kiungo huyo ambaye kwa sasa amejizolea mashabiki wengi kutokana na aina yake ya uchezaji wa kutumia nguvu.

Alipoulizwa kuhusu kupimwa na kukutwa na ugonjwa wa COVID-19 nchini Malawi, timu yake ya Taifa ya Uganda ilipokwenda kucheza, alisema ilikuwa ni hujuma, ukweli ni kwamba alipopimwa na vipimo sahihi hakukutwa na virusi hivyo na ndiyo maana alicheza mechi hiyo, akiingia kipindi cha pili.

Lwanga alisajiliwa na Simba kipindi cha dirisha dogo la usajili kuchukua nafasi ya Mbrazil Gerson Fraga ambaye alipata majeraha ya muda mrefu.

# Michezo

Jumatatu Aprili 5, 2021

Nipashe




Hazard fiti kuivaa Liverpool kesho UKURASA 22

**KWISHA KAZI...**




Kiungo wa Simba, Rally Bwalya, akishangilia na mchezaji mwenzake, Clatous Chama (Kulia), aliyemmegea pasi na kuifungia timu yake bao la tatu wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya AS Vita ya DR Congo kwenye mechi ya Kundi A ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. **MPIGAPICHA WETU**

## Namungo yapotea tena CAF nyumbani

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho, Namungo FC, jana ilijiweka kwenye mazingira magumu ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo, baada ya kuchapwa bao 1-0 dhidi Nkana FC kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Muuaji wa Namungo kwa jana alikuwa ni Diamond Chikwekwe dakika ya 69, akiunganisha pasi ndefu kutoka kwa Emmanuel Mwinde. Ni matokeo ambayo yanaifanya Namungo kushika mkia kwenye Kundi D, ikiwa haina pointi na kufungwa mechi zote tatu za mzunguko wa kwanza ilizocheza, ikicheza bila kupata bao lolote mpaka sasa, mbili ikiwa nyumbani.

Ilianza michuano hiyo kwa kufungwa bao 1-0 ugenini dhidi ya Raja Casablanca ya Morocco, kabla ya kufungwa mabao 2-0 dhidi ya Pyramids ya Misri nyumbani na kisha jana Nkana ya Zambia ikawaangukia tena.

Namungo ingeweza kuandika bao dakika ya sita tu ya mchezo, baada ya straika wake tegemeo, Mghana Steven Sey, kuachwa peke yake na mabeki wa Nkana FC wakidhani ameotea, lakini shuti lake lilipangulia na kipa Talbert Shumba na kuzua kizaazaa golini, na mabeki kufanikiwa kuuondoa.

Nkana ilitaka kususia mchezo huo kutokana na kulalamika wachezaji wao wengi kudaiwa kukutwa na maambukizo ya virusi vya corona hivyo kuwa na wanne tu wa akiba katika mchezo huo ambao ulilazimika kuchelewa na kuanza saa 11:00 jioni badala ya saa10:00 alasiri.

# AS Vita saluti kwa Simba

### ●●● Ibenge asema ni bora zaidi ya Al Ahly, atoa sababu ya kipigo, Gomes yeye afunguka...

**Na Saada Akida**

UBORA wa kikosi cha Simba na kiwango cha hali ya juu ilichokionyesha katika mechi ya Kundi A ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita, ndiyo sababu ya timu hiyo ya DR Congo kupoteza mchezo huo kwa mabao 4-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, kwa mujibu wa Kocha Mkuu wa Wakongomani hao, Florent Ibenge.

**Ibenge ambaye timu yake imekubali kipigo nyumbani na ugenini dhidi ya Simba, amesema timu yake juzi imepoteza kutokana na mambo mawili, lakini sababu kubwa ya kushindwa kupata matokeo ni ubora wa kikosi cha wapinzani wao hao.**

Akizungumza baada ya mchezo huo ambao Simba ilitawala wakati wote, Ibenge aliwapongeza wawakilishi hao wa Tanzania si tu kwa kucheza vizuri na kushinda, bali pia kuonyesha nidhamu ya hali ya juu kwenye michezo yote miwili ambayo walicheza dhidi yao, ukiwamo wa nyumbani ambao walikubali kipigo cha bao.

"Msimu huu Simba ni bora sana kuliko timu zote katika Kundi letu la A, lakini kuwapo kwa asilimilia kuwa ya wachezaji wapya pia imechangia kwetu kutofanya vizuri katika hatua hii," alisema Ibenge.

Alisema kikosi chake kinaundwa na wachezaji wengi wapya, hivyo wanarudi nyumbani kwenda kupambania kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu DR Congo baada ya kupoteza nafasi ya kutinga robo fainali.

Simba tayari imetinga robo fainali ikiwa na pointi 13 kileleni mwa msimamo wa Kundi A, ikifuatiwa na Al Ahly ya Misri yenye alama nane huku AS Vita ikifuata kwa pointi nne na Al-Merrikh ya Sudan ikiburuza mkia na alama mbili.

Kikosi cha Simba kinatarajia kuondoka nchini kesho, Jumanne kuelekea Misri kwa ajili ya mchezo wao mwisho wa hatua ya makundi utakaopigwa Ijumaa dhidi ya Al Ahly ambayo nayo imeshafuzu robo fainali.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, alisema kufanikiwa kucheza robo fainali ni juhudi za wachezaji wake kutokana na kuonyesha moyo wa upambanaji.

Gomes alisema wangeweza kufunga mabao mengi zaidi katika mchezo huo, lakini hata hivyo amefurahishwa kwa ushindi walioupata na ana kila sababu ya kuwapongeza wachezaji wake.

"Wachezaji wanastahili pongezi kwa sababu wamefanya kazi kubwa, furaha yetu pamoja na Wanasimba ni kuona tumetinga hatua ya robo fainali, huu ni muda wao wa kufurahia kwa hatua ambayo wameifikia," alisema Gomes.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >